# DALILI ZA KIAMA

## KIMEANDIKWA NA: HARUN YAHYA

### KIMEFASIRIWA NA: SHUAYBU HUSEIN KIFEA

Dalili za Kiyama Katika kipindi chote cha historia ya ulimwengu Wanaadamu wameuelewa ukubwa wa milima na upana wake, na ukubwa wa mbingu kutokana na njia zao mbali mbali za uchunguzi ijapokuwa wamekuwa na fikra potofu kuwa maumbile haya yatadumu milele. Imani hii ndio iliyozaa falsafa za kishirikina na za kilahidi za Ugiriki na dini za Sumeria za Misri ya kale. Qur'an inatuambia kuwa wale wanaoamini hivi wapo katika hatia kubwa. Miongoni mwa vitu ambavyo Mwenyezi Mungu amevibainisha katika Qur'an ni kuwa Ulimwengu umeumbwa na kwamba utakuwa na mwisho wake. Ulimwengu, kama walivyo binadamu na viumbe vingine hai, utatoweka.

Dunia hii iliyopangiliwa vizuri ambayo imefanya kazi bila kasoro kwa mabilioni ya miaka, ni kazi yake Mola ambaye ameumba kila kitu, siku moja kwa amri yake itakoma kufanya kazi. Wakati huo tayari Mwenyezi Mungu amekwisha upanga. Wakati huo ambapo ulimwengu na kila kiumbe tokea vile visivyoonekana kwa macho hadi binadamu pamoja na Nyota na Magalaksi yatasita kufanya kazi, unaitwa "Saa" katika Qur'an. "Saa" hii haina maana kuwa muda wowote bali ni neno mahususi lililotumika katika Qur'an kuelezea wakati ambao dunia itakuwa imefika mwisho wake.

Pamoja na maelezo ya mwisho wa dunia, Qur'an ina maelezo ya kina ya namna tukio zima litakavyotokea; "Mbingu zitakapopasuka," "Bahari zitakapowashwa moto," "Milima itakapoendeshwa (angani kama vumbi)" "Jua litakapo kunjwa kunjwa". Kihoro na khofu ambayo watu watakuwa nayo katika tukio hili la kutisha imeelezwa kwa kina katika Qur'an. Aya zinasisitiza kuwa hakutakuwa na pa kukimbilia wala pa kujificha. Tunachoweza kukisema hapa ni kuwa Ulimwengu utakuwa katika janga kubwa ambalo halijawahi kutokea hapo kabla.

Aya nyingi za Qur'an zinabainisha kuwa suala la mwisho wa dunia limegusa hisia za watu wengi katika kila kipindi cha historia. Katika aya kadhaa inaelezwa kuwa watu walimuuliza Mtume (s.a.w) juu ya lini utakuwa mwisho wa dunia;

Wanakuuliza juu ya Saa hiyo (yaani Kiama) kutokea kwake kutakuwa lini? (7:187),

Wanakuuliza Kiama kutokea kwake kutakuwa lini? (79:42)

Mwenyezi Mungu akamuamrisha Mtume kulijibu swali hilo hivi; Ilimu yake iko kwa Mola wangu tu. Hakuna wa kuhidhirisha wakati wake ila yeye tu (7:187).

Hii maana yake ni kuwa Allah pekee ndiye aijuaye tarehe ya siku hiyo. Kutokana na aya hii tunaelewa kuwa elimu juu ya lini utafika wakati huo imefichwa kwa wanadamu. Lazima kuna sababu maalumu kwanini Mwenyezi Mungu ameifanya siku hii kuwa siri. La muhimu ni watu kujihadhari nayo; Ambao wanamuogopa Mola wao hata wanapokuwa Faraghani, na pia hukiogopa kiama (21:49). Kwahiyo watu wachunge mamlaka ya Mwenyezi Mungu na wautafakari ukubwa wake. Kabla ya siku

hiyo ya machungu na majonzi haijawatokea kwa ghafla, watu waelewe kuwa mbali na Mwenyezi Mungu hakuna mahala pa kukimbilia. Kama siku ya mwisho ingejulikana watu walioishi huko nyuma pengine wasingelazimika kuufikiria kwa makini mwisho wa dunia, wasingejali matukio ya mwisho yaliyotajwa katika Qur'an.

Ispokuwa lazima ieleweke kuwa kuna aya nyingi zinazoelezea Saa hiyo na pale tunapozisoma tunakutana na ukweli madhubuti. Qur'an haitaji muda maalumu wa tukio hilo, bali inaelezea matukio ambayo yatatokea kabla yake. Aya hii inaelezea dalili kadhaa za saa hiyo;

Kwani wanangoja jingine ila Kiama kiwajie kwa ghafla? Basi alama zake (hicho Kiama) zimekwisha kuja. Kutawafaa nini kukumbuka wakati kitakapowajia? (47:18)

Kutokana na aya hii tunajifunza kuwa Qur'an inaelezea dalili zinazoonesha kufika kwa siku ya mwisho. Ili kuzielewa dalili hizi lazima tuzitafakari aya hizi. Vinginevyo kama aya inavyosema tafakuri yetu haitakuwa na maana pale Kiama kitakapotekea kwa ghafla. Baadhi ya hadithi za Mtume (s.a.w.w) ambazo zimetufikia zinazungumzia dalili za Kiama. Katika hadithi hizi za Mtume (s.a.w.w), kuna dalili za Kiama na maelezo ya kina kuhusu kipindi kinachokaribia kuhusu muda wa kukaribia Kiama, kipindi hiki ambacho dalili za Kiama zitatokea kinaitwa "Siku za Mwisho"

Suala la siku za mwisho na dalili za kiama, limevuta hisia za wengi katika kipindi chote cha historia ya Uislamu. Ndio maudhui makuu ya vitabu vingi vya wanazuoni na watafiti wa Kiislamu. Tunapoyakusanya pamoja maelezo yote haya, ndipo tutakapofikia hitimisho muhimu. Aya za Qur'an na hadithi za Mtume (s.a.w.w) zinaoneshakuwa kipindi cha siku za mwisho kimegawanyika katika awamu mbili:

Awamu ya kwanza: ni pale ambapo mitihani ya kiroho na mali itausibu Ulimwengu.

Awamu ya pili: inaitwa zama bora, ni wakati ambapo mafundisho ya kimaadili ya Qur'an yatatawala na kuleta ustawi bora wa mwanadamu. Zama hizi zitakapofika mwisho wake na dunia itakapoingia katika kipindi ambacho jamii zitaporomoka, Kiama kitakuwa kimefika.

Shabaha ya mfululizo huu wa mafundisho ya Qur'n ni kuzitazama dalili za Kiama kupitia aya za Qur'an na hadithi za Mtume (s.a.w.w) na kubainisha kuwa dalili hizi zimekwishaanza kujitokeza katika wakati huu tulionao.

Ule ukweli kwamba kujitokeza kwa dalili hizi kulikwisha elezwa karne 14 zilizopita umzidishie Muumini Imani kwa Allah na unyenyekevu kwake. Kitabu hiki kimetayarishwa kwa kuzingatia ahadi ya Mola wetu;

Sema sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, karibuni hivi atakuonesheni ishara zake na mtazifahamu (27:93)

Nukta yenye umuhimu makhsusi ambayo kwayo tunataka kumkumbusha msomaji ni kuwa Allah ndiye ajuaye ukweli juu ya kila kitu. Kama ilivyo katika mambo mengine yote, tunachokijua sisi kuhusu mwisho wa dunia ni kile tu ambacho Allah amekibainisha kwetu.

1

# DALILI ZA KIAMA

## SAA INAKARIBIA

Watu wengi angalau hujuwa jambo fulani kuhusu siku ya mwisho na karibu kila mmoja amesikia jambo hili au lile kuhusu kishindo cha saa hiyo. Hata hivyo wengi wanaonekana kuwa na mwenendo ule ule juu ya suaala hili kama walivyo katika masuala mengine yenye uzito mkubwa. Kwamba hawataki kulizungumzia au hata kulifikira jambo hili.

Wanajitahidi kwa kila hali kujighafilisha na khofu watakayo ipata siku ya mwisho. Hawajali ukumbusho wa siku ya mwisho uliomo katika kitabu juu ya msiba wa kuhuzunisha. Wanaepuka kuutafakari ukweli kuwa siku hiyo hapana shaka itafika. Hawataki kuwasikiliza watu wanaoizungumzia siku hii nzito au kusoma maandiko juu siku hiyo.

Hizi ni baadhi ya hila ambazo watu wamezidumisha ili kuepuka kuifikiria hatari ya siku ya mwisho. Wengi hawaamini kwa dhati kuwa saa hiyo inakuja. Tumepewa mfano wa watu hawa katika aya moja ya suratil-al-Kahf inayomzungumzia tajiri aliyemiliki bustani; ambaye alikitilia shaka Kiama;

Wala sidhani kuwa Kiama kitatokea. Na kama (kitatokea hicho Kiama) nikarudishwa kwa Mola wangu, bila shaka nitakuta kikao chema kuliko hiki (alichonipa Ulimwenguni) (18:36)

Aya hiyo inabainisha taasubi ya mtu anayemuamini Allah lakini anayekwepa kufikiria hakika ya siku ya mwisho na anatoa madai yanayopingana na aya za Qur'an. Aya nyingine inaelezea wasi wasi na mashaka yaliyowajaa makafiri kuhusiana na siku ya mwisho;

Na wale waliokufuru wataambiwa je! Hazikuwa aya zangu zikisomwa kwenu, nanyi mkajivuna na mkawa watu waovu? Na inaposemwa hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli na Kiama hakina shaka mlikuwa mkisema; hatujuwi Kiama ndio nini; hatudhani ila dhana tu wala hatuna yakini. (45:31-32).

Watu wengine ndio kabisa wanakana kuwa Kiama kipo. Wale wenye dhana hii wanatajwa hivi katika Qur'an:

Bali wanakadhibisha Kiama na tumewaandalia wanaokadhibisha Kiama Moto mkali kabisa. (Moto huo utakapowaona tokea mbali kabisa watasikia hasira yake na ngurumo yake). (25:11).

Chanzo kinachoweza kutuongoza katika njia sahihi na kutubainishia ukweli ni Qur'an. Tunapoangalia yale inayoyaelezea, tunabaini ukweli ulio dhahiri. Wale wanaojidanya kuhusu siku ya mwisho wanafanya dhambi kubwa sana, kwani Allah anabainisha katika Qur'an kuwa hakuna shaka yoyote siku ya mwisho ikaribu:

Na kwamba Kiama kitakuja, hapana shaka ndani yake;

Na kwa hakika Mwenyezi Mungu atawafufua walio makaburini (22:7) Na hatukuziumba Mbingu na Ardhi na vilivyomo ndani yake ispokuwa kwa haki. Na bila shaka Kiama kitafika (15:85)

Kwa yakini Kiama kitakuja, nacho hakina shaka lakini watu wengi hawaamini (40:59).

Yawezekana kuna watu wanaodhani ujumbe wa Quraan kuhusiana na siku ya mwisho ulifunuliwa zaidi ya miaka 1400 iliyopita na kwamba hiki ni kipindi kirefu kulinganisha na muda wa maisha ya binadamu. Lakini hapa ni suala la mwisho wa dunia, jua, nyota na kwa kifupi ulimwengu mzima. Tunapo chukulia kuwa ulimwengu una umri wa mabilioni ya miaka, karne kumi na nne ni kipindi kifupi sana cha wakati. Mwanazuoni mkubwa wa kiislamu wa zama hizi, Bediuzzaman Said Nursi alilijibu swali hilo namna hii :

Saa (ya kufika kiyama) imekaribia (54 :1) kwamba siku ya mwisho iko karibu. Hata kama ni baada ya miaka elfu moja au miaka mingi zaidi ya hii bado hili halivurugi ukaribu wake. Kwa sababu siku ya mwisho ni saa iliyopangwa kwa ajili ya ulimwengu, na katika uwiano wa maisha ya ulimwengu, miaka elfu moja au elfu mbili ni sawa na dakika moja au mbili katika mwaka. Kwa hiyo siku ya mwisho sio tu ni saa iliyopanga kwa ajili ya binadamu kwamba ionekane iko mbali sana.

Kuhubiriwa kwa mafundisho ya Qur'an ulimwenguni Katika Quran, tunakuta maneno yanayorudiwarudiwa; suna ya Allah yaani kawaida au dasturi [Sunnat Lllahi]: huu ni msemo wenye maana ya njia au sheria ya MwenyeziMungu. Kwa mujibu wa Quraan,sheria hizi hazibadiliki daima. Aya inasema: Hii ni kawaida ya mwenyezimungu iliyokuwa kwa wale waliopita zamani; walahutapata mabadiliko katika kawaida ya mwenyezimungu. (33:62)

Kanuni mojawapo ya mwenyezimungu isio badilika nikuwa, kabla ya mangamizi,kwanza jamii hupelekewa muonyaji[mjumbe].ukweli huu unabainishwa kwa maneno haya: Walahatukuangamiza mji wowote ila ulikuwa na waonyaji wa kuwakumbusha wala hatukuwa madhalim,tukawawngamiza pasina kuwapelekea waonyaji] (26:208-209). Katika historia yote, Mwenyezi Mungu ametuma muonyaji au mkumbushaji kakika kila jamii iliyokengeuka, akiwalingania kufuata njia sahihi. Sasa wale walio endelea nauovu wao ndio walio angamizwa baada ya kutimiza ule muda waliopangiwa na wakawa fundisho kwa vizazi vilivyo fuata. Tunapo iangalia kanuni hii ya mwenyezi Mungu siri nyingi muhimu zina bainika kwetu . Siku ya mwisho ni msiba wa mwisho utakao ukumba ulimwengu. Quraan ni kitabu cha mwisho cha mwenyezi Mungu kilichoshushwa kuwanasihi walimwengu. Muongozo wa Qur'an utabakia hadi mwisho wa dunia. Moja ya aya zake inasema-

Hayakuwa haya ila nimawaidha kwa watu wote (6:90). Wale wanaodhani kuwa Qur'an inazungumzia wakati au mahali fulani wanakosea sana kwasababu Qur'an ni wito wa jumla kwa walimwengu wote. Tokea wakati wa Mtume (s.a.w.w) ujumbe wa Qur'an ulikwishaenea duniani kote. Kutokana na maendeleo ya makubwa ya Teknolojia ya zama zetu,Qur'an yaweza kusambazwa kwa wanadamu wote. Hivi leo, sayansi, elimu, mawasiliano na usafilishaji vinafikia hatua ya mwisho ya maendeleo yao hasa hasa tekinolojia ya kompiuta na mtandao wa Internent, watu katika sehemu mbalimbali wanaweza kubadilishana taarifa papo kwa hapo.

Mapinduzi ya sayansi na tekinolojia yameunganisha mataifa yote ya dunia nzima maneno kama utandawazi (Globolization) yameongezwa katika msamiati. Kwa kifupi vikwazo vyote vinavyo kwaza umoja wa walimwengu vinaondoshwa kirahisi tu. Kwakuzingatia ukweli huu ni rahisi kusema kuwa katika zama zetu hizi za mawasiliano ya papo kwa hapo, Mwenyezi Mungu ameweka aina zote za maendeleo ya tekinolojia kwa manufaa yetu ni jukumu la Waislamu kutumia vema tekinolojia hizi kwa ajili ya dawa katika maisha yote ili watu wayapate mafundisho ya Qur'an.

2

# DALILI ZA KIAMA

## MITUME

Tumezungumzia kanuni zisizobadilika ambazo zimewekwa na Allah tokea kuumbwa kwa ulimwengu.kanuni ya Allah nikuwa yeye hatoiadhibu jamii ambayo hajaipelekea mjumbe.ahadi hii imetolewa katika aya zifuatazo:

Na Mola wako haangamizi miji mpaka ampeleke mtume katika mji wao mkuu,awasomee Aya zetu [wakatae ndio wangamizwe]walahatuiangamizi miji mpaka watu wake wamekuwa madhalimu. (28:59)

Na sisi si wenye kuwadhibisha[viumbe]mpaka tuwapelekee mtume.(17;15).

Wala hatukuangamiza mji wowote ilaulikuwa na waonyajikuakumbusha wala hatukuwa madhalimu.(26;208-209).

Aya hizi zinabainisha kuwa Mwenyezi Mungu kuwatuma Mitume kwenye miji mikuu kuwaonya watu. Mitume hawa huyahubiri maamrisho ya Mwenyzi Mungu lakini makafiri katika kila zama wamewadhihaki Mitume hawa nakuwaita waongo,wandawazimu na kuwasingizia kila jambo. Kwa sababu hiyo Mwenyezi Mungu huziangamiza jamii zinazoendelea kuishi katika maovu. Huwapelekea mangamizi katika wakati wasiotarajia kabisa. Kuangamia kwa watu wa Nuhu , Lutwi, Aadi, Thamuud na wengine waliotajwa katika Qur'an ni mifano ya aina ya maangamizi haya.

Katika Qur'an , Mwenyezi Mungu anabainisha sababu ya kutuma mitume;nayo ni kutoa habari njema katika jamii, kuwapa watu fursa muhimu ya kuachana na imani zao potofu na kuishi kwa kufuata dini ya Allah na kuwaonya watu ili wasipate kisingizio siku ya mwisho. Aya hii ya Qur'an inasema:

Hao ni mitume waliotoa habari nzuri kwa watu , wakawaonya ili wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletwa mitume. NaMwenyezi Mungu ni mwenye nguvu na mwenye Hekima.(4:165)

Kama inavyosema aya ya 40 ya suratil Ahzab , Mtume Muhammad ni mtume wa mwisho, 'Muhammad ni mtume wa Mungu na mwisho wa mitume.'

Kwa maneno mengine, baada ya Mtume Muhammad, Wahy kutoka kwa Allah umekamilika. Hata hivyo jukumu la kuwafikishia watu ujumbe na kuwakumbusha watu limebakia kwa kila Muislamu hadi siku ya mwisho. Miongoni mwa maudhui ya Qur'an ni yale yanayohusu watu ambao Mwenyezi Mungu amewangamiza kwasababu ya uovu na uasi wao. Na mafundisho yanayopatikana kutokana na maangamizi yaliyowafika watu hao. Kuna mlingano mkubwa kati ya jamii hizo zilizopita na jamii yetu ya leo.

Hivi leo kuna watu ambao tabia na mwenendo wao wa maisha ni mbaya zaidi kuliko hata ule mwenendo mchafu wa watu wa Lut, au ule wa dhulma wa watu wa Madian au ule wa kibri na dharau wa watu wa Nuhu au ule wa uasi na uovu wa watu wa Thamud au ule wa kukosa shukrani wa watu wa Iram pamoja na jamii nyingine zilizoangamizwa. Sababu ya wazi ya

upotevu wa kimaadili wa watu hao ni kuwa walimsahau Mwenyezi Mungu na lengo la kuumbwa kwao.

Mauaji, dhulma katika jamii, ufisadi, udanganyifu na mmomonyoko wa maadili katika zama hizi vimewafikisha watu mahala pa kukata tamaa. Lakini, isisahaulike kuwa Qur'an inatutaka tusikate tamaa na rehma za Mwenyezi Mungu. Kukata tamaa na kupoteza matumaini ni mambo yasiokubalika kwa waumini. Mwenyezi Mungu ameahidi kuwa wale wanaomuabudia kwa ikhlasi bila kumshirikisha na viumbe vyake kama miungu badala yake na wanaofanya vitendo vizuri, watapata rehma yake na kunyanyuliwa katika nafasi ya juu:

Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri kuwa atawafanya Makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya Makhalifa wale waliokuwepo kabla yao na kwa yakini atawasimamishia dini yao aliyowapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo; basi hao ndio wavunjao amri zetu (24:55).

Katika aya nyingi, Qur'an inasema kuwa:

Ni kanuni ya Mwenyezi Mungu kwamba wale waja walioamini na kushikamana na dini sahihi katika nyoyo zao watafanywa warithi wa dunia hii: Na hakika tumeandika katika Zaburi baada ya (kuandika katika) Allawhul Mahfudh ya kwamba ardhi (hii) watairidhi waja wangu walio wema (21:105).

Na tutakukalisheni (nyinyi) katika nchi baada yao. Watapata haya wale waliogopa kusimamishwa mbele yangu na wakaogopa maonyo yangu. (14:14).

Na kwa yakini tumekwishaziangamiza umma nyingi kabla yenu, zilipofanya mabaya: Na waliwajia Mitume wao kwa hoja wazi wazi; lakini hawakuwa wenye kuamini. Namna hii tunawalipa watu wanaofanya uovu. Kisha tukakufanyeni nyinyi ndio wenye kushika mahala pao baada ya (kuangamizwa) hao katika ardhi ili tuone jinsi mtakavyotenda. (10:13-14). Musa akawaambia kaumu yake:

Ombeni msaada kwa Mwenyezi Mungu na subirini. Ardhi ni ya Mwenyezi Mungu, atamrithisha amtakaye katika waja wake; na mwisho mwema ni wawamchao. Wakasema: Tumeudhiwa kabla hujatufikia na (pia sasa) baada ya wewe kutujia. (Musa) akasema: Asaa Mola wenu atamwangamiza adui yenu na kukufanyeni watala katika nchi ili aone jinsi mtakavyofanya (7:128-129).

Sanjari na habari njema zilizotolewa katika aya hizo, Mwenyezi Mungu pia ametoa ahadi muhimu sana kwa waumini. Amebainisha katika Qur'an kuwa dini ya Uislamu imeshushwa kwa wanadamu ili izipiku dini zote (iwe juu ya dini zote):

Wanataka kuizima Nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao, lakini Mwenyezi Mungu amekataa hivyo ataitimiza tu Nuru yake, ijapokuwa Makafiri wanachukia. Yeye ndiye aliyemleta Mtume wake kwa uwongofu na dini ya haki ili aijaalie kushinda dini zotep; ijapokuwa watachukia hao Makafiri (9:32-33).

Wanataka kuzima Nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao na Mwenyezi Mungu atakamilisha Nuru yake ijapokuwa makafiri watachukia.

Yeye ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uwongofu na kwa dini ya haki ili kuifanya ishinde dini zote, ijapokuwa makafiri watachukia(61:8-9).

Hapana shaka kuwa Mwenyezi Mungu atatimiza ahadi zake. Muongozo ambao utazishinda Falsafa zote potofu, itikadi potofu na mafundisho ya dini potofu ni muongozo wa Uislamu. Aya zilizonukuliwa hapo juu zinasisitiza kuwa makafiri hawawezi kuzuia jambo hili lisitimie. Wakati ambao muongozo wa Uislamu utakaposimama utakuwa wakati wa upendo, ukarimu, heshima, haki, Amani na ustawi wa kila mtu. Kipindi hiki kimeitwa kipindi kitukufu kwasababu ya kushabihiana kwake na mazingira ya pepo lakini hadi sasa zama hizo bado hazijawa. Zama hizo za kheri zitakuja kabla ya siku ya mwisho; hivi sasa zinasubiri wakati wake ambao Mwenyezi Mungu ameshapanga kuwa utafika tu.

3

# DALILI ZA KIAMA

## KURUDI KWA NABII ISA DUNIANI.

Isa au Yesu (a.s) ni Mtume aliyechaguliwa na Mwenyezi Mungu. Ni mmoja kati ya Mitume wanaozungumziwa sana katika historia ya dunia. Al-hamdulillahi kipo chanzo ambacho kwacho twaweza kupembua kipi sahihi na kipi si sahihi katika yale yaliyozungumzwa juu yake. Chanzo hicho ni Qur'an, kitabu pekee cha ufunuo ambacho hakija badilishwa wala kuhujumiwa.

Katika Qur'an tunasoma ukweli huu kuhusu Nabii Issa:

Masihi Issa bin Maryam ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na ni tamko lake (4:171)

Kumbukeni waliposema Malaika: Ewe Maryam! Mwenyezi Mungu anakupa habari njema za neno litokalo kwake (la kukwambia 'zaa' utazaa). Jina lake ni masihi, Issa, mwana wa Maryam, mwenye heshima katika dunia na akhera, na ni miongoni mwa waliopelekwa mbele na Mwenyezi Mungu. (3:45)

Na (mtaje yule mwanamke) aliyejilinda, (aliyejihifadhi) nafsi yake, na tukampulizia Roho yetu na tukamfanya yeye na mwanaye kuwa miujiza kwa walimwengu (21:91).

Naye atazungumza na watu katika utoto wake na katika utu uzima wake na atakuwa katika watu wema (kabisa) (3:46).

Issa (Yesu) alifanya miujiza kadhaa. Muujiza mwingine atakaofanya ni kuwa atarudi tena duniani katika siku za mwisho na atazungumza na watu.

Kisha tukawafuatisha nyuma Mitume wetu na tukamfuatisha Issa bin Maryam na tukampa Injili (57:27).

Bila shaka wamekufuru wale waliosema, Mwenyezi Mungu ni Masihi (Issa) bin Maryam (5:72).

Na makafiri (Mayahudi) walifanya (hila dhidi yake ili kumuua) na Mwenyezi Mungu akazipindua hila zao na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa kupindua hila (3:54).

Mwenyezi Mungu hakuacha Makafiri wamuue Issa/Yesu (a.s.), bali alimtowesha na akatoa habari njema kwa walimwengu kuwa siku moja atarudi tena duniani. Qur'an inatoa maelezo ya kurejea kwa Issa kwa ishara zifuatazo:

Na kwa ajili ya kusema kwao: Sisi tumemuua Masihi Issa Mwana wa Maryam Mtume wa Mungu hali hawakumuua wala hawakumsulubu bali walibabaishiwa (mtu mwingine). Na kwa hakika wale waliohitilafiana katika suala hilo wamo katika shaka. Hawana yakini kabisa juu ya jambo hili ispokuwa wanafuata dhana tu. Na kwa yakini hawakumuua (4:157)

Bali Mwenyezi Mungu alimnyanyua kwake na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu na mwenye hekma (4:158).

Katika aya ya 55 ya suratil Al- Imran, tunasoma kuwa Mwenyezi Mungu atawaweka juu ya makafiri wale watu wanaomfuata Issa hadi siku ya kufufuliwa. Ni ukweli wa kihistoria kuwa, miaka 2000 iliyopita wafuasi wa Issa hawakuwa na nguvu za kisiasa. Wakristo ambao wameishi enzi hizo na

ambao wanaishi zama hizi wameamini itikadi nyingi potofu. Kubwa kuliko zote ni Itikadi ya Utatu.

Hivyo ni wazi kuwa hawataweza kuitwa wafuasi wa Issa kwani kama inavyoelezwa katika Qur'an, wale wanaoamini Utatu wametumbukia katika upotofu. Kwa hali hiyo katika kipindi hicho cha kuelekea kiama, wafuasi halisi wa Issa watawashinda wapotevu na wao ndio watakaotimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu iliyotolewa katika Suratil-Al Imran. Bila shaka kundi hili tukufu litajulikana pale Issa atakaporudi tena duniani. Isitoshe Qur'an inasema kuwa watu wa kitabu wote watamuamini Issa kabla hajafa:

Na hakuna yeyote katika watu waliopewa kitabu ila humuamini Issa kabla ya kifo chake. Naye siku ya kiama atakuwa shahidi juu yao (4:159). Tunasoma wazi wazi katika aya hizi bado kuna ahadi tatu zinazomuhusu Issa ambazo bado hazijatimia. Kwanza kama walivyo binadamu wengine, Issa (a.s) atakufa. Pili Watu wote wa kitabu watamuona katika umbile lake la mwili na watamtii wakati akiwa hai. Hapana shaka kuwa biashara hizi mbili zitatimizwa pale Issa atakaporudi tena kabla ya siku ya mwisho. Bishara ya tatu juu ya Issa (a.s) kuwa shahidi juu ya watu wa kitabu, hiyo itatimizwa siku ya mwisho.

Aya nyingine katika Suratil Maryamu inaelezea kifo cha Issa (a.s):

Na amani ipo juu yangu siku niliyozaliwa na siku nitakayokufa na siku nitakayofufuliwa (19:33).

Tunapoilinganisha aya hii na aya ya 55 ya suratil Al-Imran tunaweza kubaini ukweli muhimu sana. Aya ya suratil Al-Imran inazungumzia kunyanyuliwa kwa Issa. Katika aya hii hakuna taarifa inayotolewa kuwa Issa alikufa au la. Lakini katika aya ya 33 ya Suratil-Maryam, kifo cha Issa kinazungumziwa. Kifo hiki kitatokea pale Issa atakaporudi tena duniani na kuishi kwa muda fulani na kisha kufa (Allah ndiye ajuaye).

Aya nyingine inayoelezea kurejea kwa Nabii Issa (a.s) Duniani inasema:

Na (Mwenyezi Mungu) atamfunza (Isa) kitabu na kujua elimu na kujua Taurati na Injili. (3:48).

Ili kuelewa maana ya kitabu ambayo imetajwa katika lugha ya Kiarabu katika Aya hii, lazima tuziangalie aya nyingine za Qur'an ambazo zinahusiana na suala hili. Iwapo kitabu kinatajwa pamoja na Taurati na Injili katika aya moja, basi hiyo lazima iwe na maana kuwa kitabu hicho ni Qur'an. Aya ya tatu ya Suratil Al-Imrani yaweza kuwa mfano wa jambo hilo:

Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye - Mwenye uhai wa milele, na mwendeshaji wa mambo yote. Amekuteremshia kitabu kwa haki, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake. Na aliteremsha Taurati na Injili zamani - ziwe uongozi kwa watu. Na akateremsha vitabu vingine vya kupambanua baina ya haki na Batil. (3:2-4).

Kwa hali hiyo kitabu kilichozungumziwa katika aya ya 48 ambacho Nabii Issa (a.s) anatakiwa kujifunza ni Qur'an tu. Tunajuwa kuwa Nabii Issa aliijuwa Taurati na Injili katika kipindi alichokuwa duniani ambacho ni takribani miaka 2000 iliyopita. Ni dhahiri kabisa kuwa ni Qur'an atakayoisoma pale atakaporudi tena duniani. Maelezo yanayotolewa na aya ya 59 ya Suratil Al-Imrani yanaonesha usawa baina ya Issa na Adam (a.s):

Bila shaka hali ya Issa kwa Mwenyezi Mungu ni kama hali ya Adam, alimuumba kwa udongo kisha akamwambia kuwa basi akawa. Katika aya hii twaweza kuona kuwa lazima viwepo vigezo vingi vya usawa baina Manabii hawa wawili. Kama tujuavyo, Adam na Issa (a.s.) wote wawili hawakuwa na Baba. Pia twaweza kupata usawa mwingine zaidi kutokana na aya ya hapo juu ambao ni kushuka kwa Nabii Adam ardhini akitokea peponi na kushuka kwa Nabii Issa kutoka alikohifadhiwa na Mwenyezi Mungu katika zama za mwisho. Qur'an inasema hivi kuhusu Issa:

Na kwa kweli (Issa) ni alama ya kiama, msikifanyie shaka na nifuateni. Hii ndio njia iliyonyooka. (43:61).

Tunajuwa kuwa Nabii Issa aliishi karne sita kabla ya Qur'an kushushwa. Kwa hiyo aya hii haizungumzii kipindi cha kwanza cha maisha yake bali inazungumzia kuja kwake tena duniani katika zama za mwisho mwisho. Ulimwengu wa Kiislamu na wa Kikristo kwa pamoja unamsubiri kwa hamu Nabii Issa. Ujio mtukufu wa mgeni huyu utakuwa ishara muhimu ya siku ya mwisho.

Aidha ushahidi mwingine zaidi wa kurudi kwa Nabii Issa unabainishwa na neno la kiarabu, Wakahlan katika aya ya 110 ya Suratil Maida na aya 46 ya Suratil Al-Imran. Katika aya hizi tunabainishiwa haya:

Mwenyezi Mungu atakaposema: Ewe Issa Mwana wa Maryam! Kumbuka Neema yangu juu yako na juu ya Mama yako, nilipokusaidia kwa roho takatifu (Jibril), ukazungumza na watu katika Utoto wako na katika utu uzima wako (Wakahlan) (5:110).

Naye atazungumza na watu katika utoto wake na katika utu uzima wake na (atakuwa) katika watu wema (kabisa) (3:46).

Neno hili (Wakahlan) linajitokeza katika aya hizi mbili tu na linamzungumzia Issa peke yake. Neno hili limetumika kuelezea umri mkubwa zaidi wa Issa. Neno hili linazungumzia makamo baina ya miaka 30 na 50 ambacho ni kipindi cha mwisho cha ujana na mwanzo wa utu uzima. Wanazuoni wa Kiislamu wameafikiana juu ya tafsiri ya neno hili ambayo ni kipindi kinachovuka umri wa miaka 35.

Wanazuoni hawa wanaegemea hadithi iliyosimuliwa na Ibni Abasi inayosema kuwa Issa (a.s) alinyanyuliwa kwa Allah wakati alipokuwa kijana yaani mwanzoni mwa miaka ya 30 na atakaporudi tena duniani atakuwa na miaka mingine 40 ya kuishi. Issa (a.s) ataendelea kuishi hadi uzeeni baada ya kurudi duniani, hivyo basi aya hii yaweza kuchukuliwa kama ushahidi wa kurejea tena kwa Issa (a.s) duniani.

Kama ilivyokwishaelezwa, tunapoiangalia Qur'an kwa makini, tunaona kuwa neno hili Wakahlan limetumika kumuelezea Issa tu. Manabii wote wamezungumza na watu na kuwalingania kufuata dini moja sahihi. Wote kati yao walileta ujumbe wakiwa na umri mkubwa. Lakini Qur'an haisemi chochote kuhusiana na jambo hilo juu ya Mtume mwingine yeyote. Neno hili limetumika kwa Issa (a.s) tu na huu ni muujiza.

Misemo hii miwili, "katika utoto wake" na katika "utu uzima" inagusia miujiza miwili mikubwa. Muujiza wa kwanza ni kuwa Issa alizungumza wakati akiwa mtoto mchanga. Hili ni jambo ambalo halikuwahi kutokea hapo kabla na Qur'an inalielezea tukio hili la kimiujiza mara kadha wa kadha. Mara baada ya maneno haya kuzungumza na watu utotoni yanafuata

maneno kuzungumza na watu katika utu uzima. Maneno haya pia yanaelezea muujiza. Kama maneno katika utu uzima yangezungumzia maisha yake ya awali kabla hajatoweshwa na Allah, kusema kwa Issa kusingelikuwa muujiza.

Na kwa vile usingekuwa muujiza basi usemi huu usingelitumika baada ya ule usemi wa kuzungumza katika utoto au kwa namna ya kuelezea muujiza. Kwa hali hiyo ule usemi wa "katika utoto" hadi katika "utu uzima" ungetumika na ungeelezea umri wa Issa tokea pale alipoanza kusema utotoni hadi pale aliponyanyuliwa kwa Mwenyezi Mungu.

Lakini aya inatutaka tuzingatie matukio mawili makubwa ya kimiujiza. La kwanza ni lile la kuzungumza katika utoto na lingine ni lile la Issa kuzungumza katika umri wa utu uziama. Hivyo basi usemi huu wa utu uzima una maana kuwa wakati ambao utakuwa ni muujiza. Nao ni ule wakati ambapo Issa atazungumza na watu katika umri wa utu uzima baada ya kuwa amerudi tena duniani. (Allahu A'alam).

Katika hadithi za Mtume (s.a.w.w) kuna habari ya kurudi tena kwa Issa (a.s). Katika hadithi chache habari hii inazungumzwa na habari juu ya kile ambacho Issa (a.s) atakifanya pale atakapokuwa duniani. Yafaa kumkumbusha msomaji juu ya jambo moja muhimu sana. Kwamba Mwenyezi Mungu alimtuma Mtume Muhammad (s.a.w.w) kwa Walimwengu wote akiwa kama Mtume wa mwisho. Mwenyezi Mungu alimfunulia Qur'an Mtume Muhammad (s.a.w.w) na kuwataka watu wote wafuate mafundisho ya Qur'an hadi siku ya hukumu.

Issa (a.s) atarudi tena kimiujiza duniani katika zama za mwisho lakini, kama alivyosema Mtume (s.a.w.w), hatoleta mafundisho mapya. Dini sahihi ambayo Mitume wote wamefundisha ni Uislamu ambayo Isa atapaswa kuifuata pale atakaporudi duniani. Katika Qur'an na katika Hadithi hakuna utata kuwa Issa (a.s) atarudi tena duniani katika zama za mwisho. Baada ya Waislamu kusema kuwa yumkini Isa (a.s) atarudi tena Duniani, na Mumammad (s.a.w.w) ni mtume wa mwisho, hakuna mpingano kati ya mambo haya mawili; Muhammad kuwa Mtume wa mwisho na Issa kurudi tena Duniyani.

Pale Issa atakaporejea kwa mara ya pili, hatoleta Dini mpya, bali atafuata yaleyale aliyofundisha Mtume Muhammad (s.a.w.w), Qur'an na Sunnah. Al-A'llama Imam Rabbani anasema ; "Issa (a.s) atashuka toka mbinguni , lakini atafuata njia ya Muhammad". [Imam Rabbani, Vol.11, Letter 67].

Imam Nawawi kasema Isa (a.s) atarejea na kufuata njia ya Muhammad (s.a.w.w). [Al-Qawl al-mukhtasar fi a'llamat al-Mahd al-Muntanzar]. Qadi Lyad nae kasema; Isa atatawala kwa sheria aizopewa Muhammad na atahuisha mambo ambayo watu wake waliyatelekeza. [Ibin Majah].

Mwanazuoni mkubwa wa karne iliyopita Bediuzzaman Said Nursi ametoa ufafanuzi muhimu juu ya suala hili katika kitabu chake Risalel Nnuur Collection. Kwa mujibu wa ufafanuzi wake, Isa (a.s) atarudi tena Duniani katika zama za mwisho, na atazihamisha itikadi zinazopingana na Uislamu. Chini ya uongozi wake, Wakristo watasilimu, Nguvu kubwa ya wapinzani wa Dini ya Haki itaondoshwa kabisa, imani za kipuuzi zitaondoshwa, na ulimwengu utafuata Qur'an. Labda swali muhimu

linalotarajiwa kuulizwa ni je, Isa atatambuliwa namna gani? Au ni sifa gani zitakazowawezesha watu kumtambua Issa?

Jibu ni kuwa, atakuwa na dalili zote za Utume zilizotajwa katika Qur'an. Mbali na hivyo, atakuja na ishara zinazomthibitisha kuwa yeye ndiye Masihi Isa Bin Maryamu. Wakati atakapokuja hapatakuwa na hata mtu mmoja ambaye alipata kumuona hapo kabla. Ndio kusema hakutakuwa na mtu hata mmoja atakayemtambua. Hakuna atakayeweza kumtambua kwa haiba wala sauti yake. Hakuna atakayeweza kusema kuwa yeye alimjua hapo kabla kwa kiwiliwili chake au alimwona mahali fulani na hakutakuwa na hata mmoja aliyeiona familia au nduguze ili kuweza kumfananisha.

Wale wote waliomjua walikwishakufa miaka 2000 iliyopita. Maryamu (a.s), Zakariya (as), Wanafunzi(wafuasi) wake walioishi naye kwa miaka miwili ya ujumbe wake pamoja na wale wote waliokuwepo wakati wake walikwishakufa. Kama tulivyofafanua katika kurasa za mbele, kwa amri ya kun fayakun ya Mwenyezi Mungu, Isa aliweza kuja duniani bila baba. Mwenyezi Mungu anamfananisha Isa na Adamu katika aya hii:

Bila shaka hali ya Isa kwa Mwenyezi Mungu ni kama hali ya Adamu; alimuumba kwa udongo kisha akamwambia "kuwa", basi akawa(3:59).

Ayah hii inabainisha kuwa Mwenyezi Mungu alisema "kuwa" Adamu akawa na Isa pia akawa kwa nyakati tofauti. Adamu hakuwa na mama wala baba wakati ambapo Isa hakuwa na baba lakini alikuwa na mama. Lakini akirudi tena duniani mama yake hatokuwa hai. Hivyo basi, ule ubabaishaji utakaokuwa umefanywa na Masihi wa uongo zama hata zama hautakuwa na hautaleta utatanishi. Hakutakuwa na shaka Isa kama ni yeye au la. Hakuna atakayepata kisingizo kusema huyo sio Isa (a.s). Kwa kumalizia hapa ni kwamba maelezo yote yaliyotolewa yatupelekee kutanabahi kuwa muda au miadi kuhusu kurudi tena kwa Yesu duniani na mambo atakayoyafanya, hauko mbali. Ahadi ya kurejea kwa Isa iwe changamoto kwetu ya kujiandaa kukutana naye.

4

# DALILI ZA KIAMA

## UTAFITI WA ANAGA NA UVUMBUZI

Sura ya 54 ya Qur'an inaitwa "Surat al- Qamar." Kwa kiswahili qamar tafsiri yake ni mwezi. Katika aya kadhaa sura hii inatutajia maangamizi yaliyowafika watu wa Nuhu, Ad, Thamud, Lut na Firaun kwasababu walikadhibisha mawaidha ya mitume. Wakati huo huo katika aya ya kwanza ya sura hii kuna ujumbe muhimu sana unaohusiana na siku ya mwisho:

Saa (ya kufika kiama) imekaribia; na Mwezi umepasuka (54:1).

"Neno kupasuka" lililotumika katika aya hii ni tafsiri ya neno Shaqqa, ambalo katika kiarabu lina maana mbali mbali. Miongoni mwa maana hizo ni kukatua, kulima au kuchimbua ardhi. Kutoa mfano wa hili tunaweza kurejea aya ya 26 ya suratil Al-Abasa:

Hakika tumemimina maji kwa nguvu (kutoka mawinguni). Kisha tukaipasua pasua ardhi. Kisha tukaotesha humo (vyakula vilivyo) chembe chembe. Na mizabibu na mboga. Na Mizaituni na Mitende. (80:25-29).

Kwahiyo maana ya neno "Shaqqa" hapa ni kukatua, kuchimbua ardhi ili kuotesha mimea mbali mbali. Kama tutarejesha kumbukumbu zetu mwaka 1969, tutaona moja ya maajabu makubwa ya Qur'an. Majaribio yaliyofanywa mwezini mnamo Julai 20,1969 yaweza kuwa kielezeo cha kutimia kwa maneno yaliyosemwa miaka 1400 iliyopita katika Suratil Qamar.

Katika tarehe hiyo, wanaanga wa Marekani walikanyaga mwezini. Wakachimba udongo wa mwezini na kufanya uchunguzi wa Kisayansi walichukuwa sampuli ya mawe na udongo. Kwa kweli hili ni jambo lenye mvuto mkubwa kwani kitendo hiki kinawafikiana kabisa na maelezo yaliyotolewa katika aya hiyo ya 26. Kusisitiza hili ni kwamba wakati wa Mtume hakuna mtu aliyejua kama mwezini kuna udongo mithili ya ardhi. Kwahiyo kutumika kwa neno shaqqa lenye maana ya kuchimba, kuchimbua au kukatua kama lilivyotumika katika aya hiyo ya 26 kunathibitishwa na huo uchunguzi wa mwaka 1969 ambapo wanaanga waliokwenda mwezini walichimba udongo wa mwezini ndio kusema wameitimiza kwa vitendo aya hiyo ya Qur'an. Ndio maana tunasema hii ni moja ya maajabu ya Qur'an.

Wakati wanaanga hawa walipochimba udongo wa mwezini, walikusanya kilo 15.4 za sampuli ya mawe na udongo. Sampuli hizi zikaja kuvuta hisia za wengi. Kwa mujibu wa ripoti ya shirika la anga la Marekani, NASA hamasa iliyoonyeshwa na watu juu ya sampuli hizi ilivunja rekodi ya hamasa zote zilizooneshwa katika safari zao zote za angani za karne ya 20. Safari ya mwezini inaelezewa kwa kauli mbiu hii "hatua moja ndogo ya mtu mmoja ni mwendo mkubwa wa kuruka kwa wanadamu wote". Huu ulikuwa ni wakati wa kihistoria wa utafiti wa anga. Ni tukio lililochukuliwa na Kamera, na kila mtu kutoka wakati huo hadi leo amelishuhudia.

Kama ilivyoelezwa katika aya ya kwanza ya Suratil al- Qamar, tukio hili kubwa lenyewe pia laweza kuwa ishara ya siku ya mwisho. Yaweza kuwa ishara kuwa ulimwengu upo katika siku za mwisho kabla ya hukumu. (Allahu A'alam). Mwisho hatuna budi kuzingatia kuwa kuna onyo kubwa kufuatana na aya hizi. Kuna ukumbusho kuwa ishara hizi zinatoa fursa

muhimu kwa watu kuacha mwendo mbaya na kwamba wale wasiozingatia onyo hili basi watapata fadhaa kubwa pale watakapofufuliwa siku ya hukumu ambayo katika Qur'an inaelezewa kama siku yenye huzuni isiyoelezeka:

Saa (ya kufika Kiama) imekaribia na Mwezi umepasuka. Na wakiona muujiza hugeukia upande mwingine na kusema uchawi tu unazidi kuendelea! Ndio wamekadhibisha hivi na wamefuata matamanio ya nafsi zao. Na kila jambo ni lenye kuthibiti. Na kwa yakini zimewajia habari zenye makatazo makubwa. Zenye hikma kamili lakini maonyo kwao hayafai kitu. Basi jiepushe nao. Na wakumbushe siku atakapoita mwiitaji huyo kuliendea jambo zito (la kiama). Macho yao yatainama chini, wanatoka katika makaburi kama kwamba ni Nzige waliotawanyika, wanamkimbilia muhitaji huyo na huku wanasema hao makafiri: Hii ni siku ngumu kabisa. (54:1-8).

Miaka 1400 iliyopita Mtume Muhammad (s.a.w.w) alitoa bishara nyingi kuhusiana na siku za mwisho na akaelezea maono yake juu ya wakati huo kwa maswahaba wake. Maneno haya muhimu yamerithishwa kwa vizazi na vizazi hadi kufikia leo hii. Yamo katika vitabu vya hadithi na katika maandiko ya wanazuoni wa Kiislamu.

Hadithi ambazo tutazinukuu katika kitabu hiki zina bishara hizo zilizotolewa na Mtume (s.a.w.w). Labda yaweza kuzuka shaka kwa msomaji kuhusiana na ukweli na usahihi wa hadithi hizi zinazozungumzia mwisho wa dunia. Ni ukweli unaofahamika kuwa, huko nyuma kulikuwa na hadithi nyingi za kughushi ambazo zilidaiwa kuwa za Mtume (s.a.w.w) lakini hadithi zinazoelezea mada yetu hii zitatambuliwa kirahisi kuwa zilitoka kwa Mtume (s.a.w.w).

Kuna utaratibu wa kutofautisha hadithi sahihi na hadithi zisizo sahihi. Kama tujuavyo hadithi zinazozungumzia zama za mwisho zinahusiana na matukio yatakayotokea baadaye. Kwasababu hii pale hadithi inapothibiti kulingana na wakati, shaka zote juu ya chanzo chake huondoka.

Wanazuoni kadhaa wa Kiislamu waliofanya utafiti juu ya mada ya zama za mwisho na juu ya dalili za kiama wametumia kigezo hiki. Mwana taaluma wa fani hii, Ulamaa Bediuzzaman Said Nursi amesema kuwa ule ukweli kwamba hadithi zinazohusu zama za mwisho zimeshabihiana na matukio na mambo yaonekanayo katika zama zetu unabainisha ukweli wa hadithi hizo. Baadhi ya dalili zilizotajwa katika hadithi ziliweza kuonekana katika baadhi ya maeneo ya dunia katika wakati wowote ule wa historia ya miaka 1400 ya Uislamu.

Lakini hilo pekee lisingeliweza kuthibitisha kuwa kipindi hicho kilikuwa zama za mwisho. Ili kipindi kiitwe cha zama za mwisho basi zile dalili zote za siku ya mwisho lazima zionekane na zitokee katika kipindi hicho hicho. Hii inaelezwa katika hadithi: Dalili zinafuatana moja baada ya nyingine kama vile shanga za mkufu zinavyoanguka moja baada ya nyingine pale kamba yake inapokatika (Tirmidhi).

Tunapoziangalia zama za mwisho kwa kuzingatia maelezo yaliyotolewa hapo juu, tunaibuka na hitimisho la kuajabisha. Dalili ambazo Mtume (s.a.w.w) alizielezea kwa kina zinatokea, hivi leo moja baada ya nyingine katika kila pembe ya dunia kama vile vile zilivyoelezwa. Kwahiyo hadithi moja kwa moja zinatoa picha kamili ya wakati wetu. Huu kwa hakika ni

muujiza unaohitaji mazingatio makubwa sana. Kila dalili inayotokea inawakumbusha watu kuwa zama za mwisho zimekaribia, ile siku ambayo watu watatoa wenyewe hesabu ya amali zao mbele ya Mwenyezi Mungu. Hivyo basi watu wanapaswa kurejea upesi upesi katika maadili ya Qur'an.

5

# DALILI ZA KIAMA

## VITA NA MACHAFUKO

Katika Hadithi moja Mtume (s.a.w.w) alizielezea zama za mwisho hivi: Mtume wa Allaha alisema:

Harji (itazidi kuongezeka), Watu wakauliza harji ndio nini? Akajibu, ni mauaji, ni mauaji. (Bukhari). Maana ya harji iliyotajwa katika hadithi ya hapo juu ya Mtume (s.a.w.w) ni "machafuko makubwa" na "vurugu" ambavyo havitaishia mahala pamoja bali vitaenea duniani kote.

Pia kuhusiana na swala hili maneno mengine ya Mtume yanasema:

Ile saa itafika wakati vurugu, umwagaji damu na machafuko yatakapokuwa mambo ya kawaida. (Al-Muttaqi Al-Hindi, Muntakhab Kanzul Ummaal) Ulimwengu hautakoma mpaka zije enzi ambapo kutakuwa na mauaji makubwa na umwagaji mkubwa wa damu (Muslim).

Tukizitafakari Hadithi hizo, tunafikishwa katika hitimisho muhimu. Mtume (s.a.w.w) alielezea mitafaruku, fujo, mauaji na vita vitavyoikumba dunia nzima na kuenea kwa hali ya khofu na akabainisha kuwa matukio haya ni ishara ya Kiama.

Tukiangalia katika karne 14 zilizopita, twaona kuwa vita vilikuwa vya Kinchi kabla ya karne 20. Hata hivyo vita ambavyo vimemuathiri kila mtu duniani, vilivyoathiri mifumo ya siasa, na mifumo ya uchumi na jamii, vimerindima zaidi katika nyakati za karibuni hususan katika vita kuu mbili za dunia.

Katika vita kuu ya kwanza ya dunia zaidi ya watu Milioni 20 walikufa, na katika vita kuu ya pili ya dunia, zaidi ya watu Milioni 50 waliuawa. Vita kuu ya pili ya dunia ndiyo inayotambuliwa kuwa ni vita iliyomwaga damu nyingi mno, iliyokuwa kubwa mno na iliyoleta maangamizi makubwa katika historia.

Teknolojia ya sasa ya Kijeshi ikiwa ni pamoja na Silaha za Kibaolojia, Kikemia na Nyuklia ndio iliyozidisha madhara ya vita katika kiwango ambacho hakijapata kutokea katika historia. Kutokana na silaha za maangamizi ambazo zimezidi kuboreshwa, inakubaliwa na wengi kuwa Ulimwengu hautaingia katika vita ya tatu ya dunia.

Migogoro ambayo imetokea baada ya vita kuu ya pili ya dunia, vita baridi, vita vya Korea, vita ya Vietnam, mgogoro wa Warabu na Waisrael vita vya Ghuba na Iraq ni miongoni mwa matukio mabaya sana ya wakati wetu. Hali kadhalika vita vya kieneo, migogoro na vita vya wenyewe kwa wenyewe vimesababisha maangamizi makubwa katika sehemu nyingi za dunia. Katika nchi kama Bosnia, Palestina, Chechnya, Iraq, Afghanistan, Kashmiri na sehemu nyingine nyingi, matatizo haya bado yanaendelea kumkumba mwanadamu.

Mfano mwingine wa machafuko yanayomuathiri mwanadamu mithili ya vita ni Ugaidi unaoratibiwa kimataifa kama wanavyokubali viongozi wengi kuwa vitendo hivi vya Ugaidi vimeongezeka mno katika nusu ya pili ya karne ya 20. Kwa kweli yawezekana kusema kuwa Ugaidi ni jambo makhususi la karne ya 20.

Jamii zilizobobea katika ubaguzi, Ukomunist na Itikadi nyingine kama hizo au zenye malengo ya Utaifa zimeshiriki katika vitendo vya kinyama kwa msaada wa teknolojia ya leo. Katika historia ya karibuni tu, vitendo vya Ugaidi mara kwa mara vimeleta maangamizi. Damu nyingi imemwagika na watu wasio na hatia ama wamejeruhiwa au wameuawa lakini bado wanadamu hawajapata fundisho kutokana na matukio haya ya balaa. Katika nchi nyingi za dunia Ugaidi unaendelea kuwa msingi wa tawala na sera.

Kuna aya nyingi katika Qur'an zinazohusiana na jambo hili. Katika Surati Arum inaelezwa kuwa machafuko yameikumba dunia kwasababu ya yale ambayo watu wameyafanya kwa mikono yao:

Uharibifu umedhihiri barani na baharini kwasababu ya yale iliyoyafanya mikono ya watu ili awaonjeshe adhabu ya baadhi ya mambo waliyoyafanya, huenda wakarudi (wakatubia kwa Mwenyezi Mungu) (30:41). Hatuna budi kusema kuwa aya hii inatukumbusha ukweli muhimu sana. Machungu na Masahibu yanayotokana na makosa ya wanadamu yanatupa fursa ya kutanabahi na kuepuka kuyarudia.

6

# DALILI ZA KIAMA

## KUANGAMIA KWA MIJI MIKUU:

Vita na majanga Miongoni mwa mambo aliyoyasema Mtume kuhusiana na zama za mwisho ni hili:

Miji mikuu itaangamia na itakuwa kana kwamba haikupata kuwepo hapo kabla (Al-Muttaq Al-Hindi Al Burhan fi Alamat Al Mahadi Akhir al Zaman)

Kuangamia kwa miji mikuu iliyozungumzwa katika hadithi hii kunatukumbusha maangamizi ambayo yanatokea hivi leo kutokana na vita na majanga mbali mbali ya asili. Silaha za kisasa za Nyuklia, Madege ya Kivita, Mabomu, Makombora na Zana nyingine za kisasa zimesababisha maangamizi yasiyosemeka.

Zana hizi za hatari zimeleta kiwango kikubwa cha maangamizi ambacho dunia haijapa kukiona hapo kabla. Kwahakika miji mikuu ndio imekuwa malengo makuu ya mashambulizi na imekuwa ikiathirika zaidi kutokana na maangamizi haya. Maangamizi yasiyo na mfano ya vita ya pili ya dunia ni kielezeo cha haya. Kwa kutumika bomu la Atomic katika vita kuu ya dunia, miji ya Hiroshima na Nagasaka iliangamizwa kabisa.

Kutokana na Mabomu mazito, miji mikuu ya Ulaya na miji mingine mikubwa imepata kiwango kikubwa cha hasara. Buku la marejeleo (Encylopedia Britannica) linaelezea hasara iliyosababishwa na vita kuu ya pili ya dunia katika miji ya Ulaya: Maangamizi yaliyotokea yameigeuza sehemu kubwa ya Ulaya kuwa kama taka taka na ilimalizwa na mabomu ya moto, bara bara zilijaa mashimo matupu, sura ya nchi ilikuwa giza tupu njia za reli zikaharibiwa na kutofanya kazi, madaraja yalibomolewa na bandari zilijaa Meli. Berin, anasema Jenerali Lusias D. Clay, Naibu Gavana wa Jeshi katika ukanda wa Post war German, lilikuwa kama jiji la wafu.

Kwa kifupi maangamizi ambayo yalisababishwa na vita ya pili ya dunia yanashabihiana kabisa na hadithi ya Mtume (s.a.w.w). Sababu nyingine ya maangamizi ya miji mikuu ni majanga ya asili. Ni ukweli wa kitakwimu kuwa zama tunazoishi hivi leo zimeshuhudia kuongezeka kwa idadi na madhara ya majanga ya asili. Katika miaka kumi iliyopita, majanga ya asili yaliyosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa yalikuwa ni mambo ambayo hayakuwahi kutokea.

Maangamizi, Umasikini, mauaji, machafu kuongezeka Sababu nyingine ya maangamizi katika miji ni majanga ya asili. Kulingana na takwimu, zama zetu zimeshuhudia ongezeko la idadi na ukubwa wa majanga ya asili. Katika kipindi cha miaka kumi iliyopita kulikuwa na majanga yaliyosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa. Haya yalikuwa ni majanga ya aina yake.

Hatari kubwa ya uchafuzi wa hali ya hewa unaosababishwa na viwanda ni tishio kwa dunia nzima. Viwanda vinavuruga urari wa angahewa ya dunia na kuongeza mabadiliko ya hali ya hewa. Mwaka 1998 ulikuwa ni mwaka wa joto kali sana duniani tangu rekodi za hali ya hewa zianze kuwekwa. Kwa mujibu wa maelezo ya kituo cha taarifa za hali ya hewa cha Marekani, idadi kubwa ya majanga yaliyotokana na hali ya hewa ilikuwa mwaka huo wa 1998.

Kwa mfano, Kimbunga kimeelezewa na wachunguzi wengi kuwa ndio janga baya mno la kimaumbile lililoikumba Amerika ya kati. Katika miaka michahe iliyopita vimbunga, dhoruba, tufani na majanga mengine yameleta maangamizi katika bara la Amerika na katika sehemu nyingine kadha wa kadha za dunia. Mbali na hayo mafuriko nayo yameleta maangamizi katika maeneo kadhaa ya watu. Aidha mitetemeko ya ardhi, Volkeno nayo pia yamesababisha maangamizi makubwa. Hivyo basi maangamizi yote haya yaliyotokea katika miji ni ishara muhimu.

Mitetemeko ya ardhi Hapana shaka kuwa katika historia, hakuna majanga ya asili ambayo yamewaathiri watu kwa kiasi kikubwa kama mitetemeko ya ardhi. Mitetemeko ya ardhi hutokea mahali popote na wakati wowote. Kwa karne zote mitetemeko ya ardhi imesababisha maafa na hasara kubwa ya mali. Kwa sababu hii tetemeko la ardhi ni janga linalohofiwa mno. Hata teknolojia ya karne ya Ishirini na Ishirini na moja imeweza kwa kiasi kidogo sana kuzuia uharibifu wa tetemeko la ardhi.

Tetemeko la ardhi la mwaka 1995 kule Kobe laweza kuwa somo kwa wale wanaodhani kuwa teknolojia itaweza kudhibiti maumbile. Itakumbukwa kuwa tetemeko hili la ardhi lilitokea bila kutarajiwa kwenye eneo kubwa la viwanda na usafirishaji. Licha ya ukweli kwamba lilidumu kwa sekunde ishirini tu, kama lilivyoripoti gazeti la Time, bado lilisababisha hasara ya dola bilioni 100. Kadhalika tetemeko la ardhi ndani ya bahari lililofahamika kama Tsunami fukweni mwa nchi za Indonesia, Thailand na ukanda mzima wa Pwani ya Asia, lilikuwa la aina yake kupata kutokea katika historia ya mwanaadamu.

Katika miaka michache iliyopita mitetemeko mikubwa ya ardhi imetokea mara kwa mara na ndio matishio makubwa ya maisha ya watu duniani kote. Tukiangalia takwimu zilizokusanywa na kituo cha taarifa za matetemeko ya ardhi cha Amerika mwaka 1999 tunaona kuwa mitetemeko ipatayo 20, 832 ilitokea sehemu mbali mbali duniani. Matokeo yake watu wanaokadiriwa kufikia 500,000 walikufa. Matukio yote haya yanakumbushia maneno ambayo Mtume (s.a.w) aliyasema miaka 1400 iliyopita: Kiama hakitasimama mpaka pale mitetemeko ya ardhi itakapotokea mara kwa mara. (Bukhari).

Katika Qur'an kuna aya kadhaa zinazobainisha uhusiano kati ya mitetemeko ya ardhi na zama za mwisho. Sura ya 99 inaitwa suratil Zil Zaala ambayo maana yake ni mtikisiko au tetemeko la ardhi. Sura hii yenye aya nane inaelezea mtetemeko mkubwa wa ardhi na inasema kuwa kufuatia mtetemeko huo siku ya hukumu itakuwa imefika. Watu watafufuliwa makaburini na kutoa hesabu ya amali zao kwa Mwenyezi Mungu na kupata malipo yao hata kwa jambo dogo sana walilolifanya:

Itakapotetemeshwa ardhi kwa mtetemesho wake mkubwa. Na itakapotoa ardhi mizigo yake, na binadamu akasema (wakati huo) (oh!) ina nini leo ardhi? Siku hiyo itatoa habari zake zote kwa kuwa Mola wake ameifunulia (ameiamrisha kufanya hayo). Siku hiyowatu watatoka (makaburini) vikundi vikundi ili waonyeshwe vitendo vyao. Basi anayefanya wema hata kwa kiasi cha uzito wa mdudu chungu ataona jazaa yake na anayefanya uovu hata kwa kiasi cha uzito wa mdudu chungu ataona jazaa yake. (99:1-8).

7

# DALILI ZA KIAMA

## UMASIKINI

Inafahamika kuwa umasikini ni ukosefu wa chakula, makazi, mavazi, huduma za afya na mahitaji mengine ya msingi kwa sababu ya kipato duni. Licha ya fursa zinazopatikana kutokana na maendeleo ya teknolojia, umasikini hivi leo ni moja kati ya matatizo makubwa kabisa yanayoukabili ulimwengu. Katika mabara ya Afrika, Asia, Amerika Kusini na Ulaya Mashariki watu wengi wanahangaika na njaa kila siku. Kwa sababu ya mgao mbaya wa rasilimali za ulimwengu umasikini umesababisha uwepo mgawanyiko kati ya nchi za kaskazini ya jangwa la sahara ambazo ni za ulimwengu wa kwanza na nchi za kusini maskini ambazo ni za ulimwengu wa tatu.

Ubeberu na Ubepari usio na mipaka unazuia mgawanyo wa kipato ulimwenguni kote na unakwaza maendeleo ya nchi changa na nchi zinazoendelea. Wakati ambapo kuna watu wachache wanaofurahia kipato kinachozidi mahitaji yao, kuna idadi kubwa ya watu wanaohangaika na matatizo ya umasikini na ufukara. Katika Ulimwengu wa leo umasikini umefikia hatua mbaya au kiwango kibaya sana.

Ripoti ya mwisho ya UNICEF ilieleza kuwa mmoja kati ya kila watu wanne duniani anaishi katika tabu na shida isiyoelezeka. Watu bilioni 1.3 duniani wanaishi kwa wastani wa chini ya dola moja kwa siku. Watu bilioni 3 duniani wanaishi kwa dola mbili kwa siku. Takribani watu bilioni 1.3 hawapati maji safi. Watu bilioni 2.6 hawapati maji salama.

Kwa mujibu wa ripoti ya shirika la chakula duniani, (FAO), Mwaka 2000, watu milioni 826 duniani kote hawapati chakula cha kutosha. Kwa maneno mengine mmoja katika kila watu sita ana njaa. Katika miaka kumi iliyopita dhulma katika mgawanyo wa kipato imeongezeka kwa kiwango kisichosemeka.

Ripoti za umoja wa Mataifa zinaonesha kuwa, katika mwaka 1960 asilimia 20 (20%) ya watu wanaoishi katika nchi tajiri kabisa duniani walikuwa na pato lilozidi mara thelathini pato la nchi 20 masikini kabisa. Hadi kufikia mwaka 1995 iliongezeka mara 82. Kikiwa ni kielezeo cha kutoweka kwa haki ulimwenguni, mali za matajiri 225 wakubwa kabisa ulimwenguni ni sawa na pato la mwaka la asilimia 47 (47%) ya nchi masikini ulimwenguni.

Takwimu za sasa zinaonyesha yale ambayo Mtume (s.a.w.w) aliyasema juu ya kuongezeka kwa umasikini. Katika hadithi inabainishwa kuwa umasikini na njaa ni miongoni mwa dalili za kipindi cha kwanza cha zama za mwisho:

Masikini wataongezeka (Amal Al Diin Al Qazwin, Mufid Al Ulum wa Mubid Al humum) Kipato kitagawanywa kwa matajiri tu, hakuna mafao kwa masikini. (Tirmidhi). Ni dhahiri kuwa kipindi hicho kilichobashiriwa na Mtume (s.a.w.w) kinawiana na hali ya wakati wetu wa leo. Tukiangalia karne zilizopita tunaona kuwa shida na tabu zilizoletwa na ukame, vita na majanga mengine zilikuwa za muda mfupi na ziliishia katika eneo moja moja. Lakini umasikini na shida za leo ni za kudumu na sugu. Kwa hakika

Mola wetu ni Mwingi wa Rehma, yeye hadhulumu watu lakini kwa sababu ya ukosefu wa shukurani wa wanadamu na maovu wanayoyafanya, umasikini na tabu vimeongezeka. Kwa hakika hali ya mambo ya kusikitisha inaonesha wazi kuwa dunia imetanzwa na uchoyo na ubinafsi.

Kuporomoka kwa maadili, kushamiri kwa ushoga na ukahaba Katika zama zetu za leo kuna janga kubwa linalohatarisha uhai wa jamii ulimwenguni. Mithili ya virusi vinavyoua mwili, janga hili linasababisha msiba mkubwa wa kijamii. Janga hilo ni mmomonyoko wa maadili ambayo husaidia kustawisha jamii. Ushoga, Ukahaba, uhusiano haramu wa kijinsia kabla ya ndoa na nje ya ndoa, Filamu za ngono, Picha za ngono, unyanyasaji wa kijinsia na ongezeko la maradhi ya zinaa, mashindano ya kukaa uchi maarufu ulimbwende, uuzaji na utumiaji wa vileo na dawa za kulevya miongoni mwa vijana ni miongoni mwa ishara kubwa za kuporomoka kwa maadili.

Mambo haya ndiyo yamekuwa yakizishughulisha jamii. Idadi kubwa ya watu haijali hatari hii inayozidi kuwa kubwa na wanaiona kama jambo la kawaida tu. Lakini takwimu zinaonesha kuwa kila siku ipitayo kiwango cha hatari kinazidi kuongezeka. Ongezeko la maradhi ya zinaa ni kigezo kikuu cha kusaidia kuonesha ukubwa wa matatizo yanayomkabili mwanadamu. Kwa mujibu wa rekodi za Shirika la Afya ulimwenguni magonjwa yanayotokana na zinaa yanachukuwa sehemu kubwa ya maradhi. Ripoti zinaonesha kuwa kati ya kesi mpya za magonjwa ya zinaa zinazokadiriwa kufikia milioni 333 kila mwaka ulimwenguni kote, Ukimwi ndio tatizo kubwa zaidi.

Takwimu za Shirika la Afya ulimwenguni (WHO) zinaonesha kuwa idadi ya vifo vinavyotokana na ugonjwa wa Ukimwi tokea pale ulipoanza imefikia watu milioni 18.8. Ripoti za shirika hilo kwa mwaka 2000 zinaielezea hivi hali ya mambo: "Ukimwi una nafasi ya kipekee katika kuleta athari mbaya za kijamii, kiuchumi na katika mipango ya sensa ya maendeleo".

Miongoni mwa mambo mabaya kabisa yanayozidi kushamiri ni ushoga. Katika baadhi ya nchi jambo hili limehalalishwa kama ndoa, linapewa heshima zote za ndoa na limeundiwa vyama na jumuiya. Duniani kote uovu huu unapingwa. Kushamiri kwa ushoga hivi leo kunatukumbusha hatima ya watu wa Lut waliokithiri katika uovu huu. Kama isemavyo Qur'an walipoukataa wito wa Lut kuiendea njia sahihi, Mwenyezi Mungu aliuangamiza mji na watu wake kwa maangamizi makubwa.

Ni dhahiri kuwa zile hadithi zinazoelezea zama za mwisho na mporomoko wa maadili zinathibitika hivi leo. Hadithi moja inasema kuwa kutoweka kwa aibu katika dhambi ya ukahaba ni dalili ya kiama:

Kutashitadi maingiliano haramu ya kijinsia wazi wazi (Bukhari). Saa hiyo itafika wakati uzinzi utakapokuwa umeenea sana (Al-Haythami, kitab al fitan) Kufifia kwa maadili na hisia ya aibu kunaelezwa kwa maneno haya:

Saa ya mwisho haitasimama hadi pale watu watakapofanya uzinzi njiani (njia wanazopita watu) ( Ibn Iban na Bazzar). Yafaa kukumbuka kuwa hivi sasa matukio ya ukahaba yanayochukuliwa na kamera za siri yamekuwa yakioneshwa katika Internate, vituo vya Televisheni na katika magazeti yanayoitwa ya ngono na udaku. Makahaba wanaingiliana na wateja wao

wazi wazi katikati ya mitaa. Hali kadhalika kuna Filamu na picha nyingi zinazosambazwa ulimwenguni kote ambazo zinaonesha uzinzi unavyofanyika wazi wazi. Takriban katika miji mingi duniani makahaba wamekuwa wakisimama na wateja wao na kufanya mambo ya ajabu barabarani hasa nyakati za usiku.

Hii ni dalili nyingine ya kiama iliyobainishwa katika hadithi. Mamilioni ya watu wanaishuhudia wenyewe dalili hii duniani kote. Hadithi zifuatazo zinaonyesha kuwa kuibuka kwa ushoga kuwa jambo la kawaida la maisha ni ishara kuu ya zama zinazokaribia siku ya mwisho:

Wanaume watawaiga wanawake na Wanawake watawaiga wanaume. (Allama Jalaluddin Swiyuti, Durre- Mansuri). Watu watazama katika ushoga na usagaji (Al Mutaqi al Hindi, Muntakhab, Kanzul Ummaal).

Vitendo vya wanaume kuwaiga wanawake na wanawake kuwaiga Wanaume vimekuwa vingi hivi leo. Tunashuhudia Wanaume wanaosuka nywele zao na pia tunashuhudia Wanaume wanaowasuka nywele wanawake kwenye Masaluni na majumbani. Imekuwa ni aina ya ajira kwa wanaume hawa hasa Wamasai kupita mitaani kusuka nywele akina Mama.

Pia tunashuhudia Wanaume wakivaa hereni masikioni na vidani shingoni. Tunashuhudia teknolojia ikitumika vibaya kubadilisha maumbile ambako kumeleta kiroja cha mwanaume kubeba uzazi na kujifungua! Kwa upande mwingine tunashuhudia Wanawake wakivaa mavazi ya Wanaume, wakijaribu kuiga usemaji wa kiume. Wakioa wanawake wenziwao na wakifanya kazi za mitulinga. Tunashuhudia wanawake wakivaa mavazi yenye kuonesha vivazi vyao vya ndani na maungo mateke ili kushawishi uzinzi.

8

# DALILI ZA KIAMA

## KUKANUSHA DINI SAHIHI NA MAADILI YA QUR'AN

Hadithi zinazozungumzia dalili za siku ya mwisho zinatupa maelezo ya kina juu ya wakati ambao dalili hizi zitadhihirika. Twaweza kufahamikiwa kutokana na hadithi za Mtume (s.a.w.w) kuwa awamu ya kwanza ya zama za mwisho ni kipindi ambacho kitaonekana kuwa cha kidinidini, lakini kumbe ni kipindi ambacho kitaikataa kabisa dini ya Allah na maadili ya Qur'an.

Ni kipindi ambacho yale mambo yaliyobainishwa katika aya za Qur'an yatafumbiwa macho, dini itatumbukia katika mifarakano, migogoro, hamasa na ushabiki. Ibada zitafanywa kwa ria na dini itatumika kama biashara ya kujipatia faida na maslahi ya kidunia. Ni katika kipindi hiki ambapo Imani haitategemea elimu na utafiti bali itakuwa mwigo wa kufuata mkumbo tu na hamasa ya mtu. Katika kipindi hiki watu wanaoitwa Waislamu watakuwa wengi mno wakati ambapo wanazuoni wa kweli na Waislamu wenye Ikhlasi watakuwa wachache mno.

Zifuatazo ni dalili zilizotajwa na Mtume (s.a.w.w) Karne 14 zilizopita, dalili ambazo zinathibitika wazi wazi katika wakati tulionao: Kwa mujibu wa Qur'an, Mtume (s.a.w.w) anasema kuwa watu wake wameitelekeza Qur'an:

Na Mtume alikuwa akisema, Ewe Mola wangu! Hakika watu wangu wameifanya Qur'an hii kuwa kitu kilichoachwa. (25:30). Inabainishwa katika hadithi kuwa katika zama za mwisho muongozo wa Qur'an utatupiliwa mbali na watu watajitenga nao:

Karibia ya kusimama kwa saa kutakuwa na zama ambazo elimu ya (Qur'an) itatoweka na giza totoro litagubika (Bukhari).

Utakuja wakati wa uma wangu ambapo hakutabaki chochote kilichobaki katika Qur'an isipokuwa sura yake ya nje tu na hakutabaki chochote cha Uislamu isipokuwa jina lake tu na wao watajiita kwa jina hili ingawaje ni watu waliombali kabisa na Uislamu. (Ibn Babuya, Thawab ul-A'amal). Mfano umetolewa katika suratil Jumaa aya 5:

Mfano wa wale waliopewa Taurat, kisha hawakuichukua kwa ktuitumia ni kama Punda anayebeba vitabu vikubwa vikubwa.

Hapana shaka kuwa aya hii inatoa onyo kwa Waislamu, ikiwakumbusha kuwa wajihadhari wasije wakatumbukia katika dhambi ileile nzito. Qur'an imeshushwa kama kitabu cha muongozo ambao watu waufuate.

Mtume (s.a.w.w) kasema kuwa licha ya ukweli kuwa Qur'an itasomwa lakini elimu na hekima iliyomo ndani yake hatazingatiwa. Hii ni dalili nyingine ya ule wakati wa zama za mwisho:

Utakuja wakati juu ya umma ambapo watu watasoma Qur'an lakini haitakwenda kokote isipokuwa itaishia kwenye makoo yao (haitaingia nyoyoni.) (Bukhari).

Mtume wa Allah alisema jambo fulani kisha akasema utatokea wakati ambapo elimu haitakuwepo tena. Aliuliza Ziyadi: Ewe Mtume wa Allah itatowekaje elimu licha ya ukweli kuwa tutakuwa tukiisoma Qur'an na kuwafundisha watoto wetu kuisoma na watoto wetu nao watawafundisha

watoto wao kuisoma hadi siku ya kufufuliwa? Hapo Mtume akasema je Mayahudi na Wakristo hawasomi Taurati na Biblia na kutotenda kwa mujibu wa yale yaliyomo humo? (Ahmad, ibn Majah, Tirmidhi).

Watu kuitumia dini kwa malengo ya kidunia na kujivika ngozi ya kondoo waonekane wema. Kufuata maadili ya Wayahudi na Wakristo Ni dalili moja wapo ya kiama kuwa baadhi ya Waislamu watafuata nyendo za Wayahudi na Wakristo tena watawaiga kimasonge. Mtume (s.a.w.w) kasema:

"Kwa hakika mtafuata nyendo za watu waliokuwepo kabla yenu shubiri kwa shubiri na dhiraa kwa dhiraa (Inchi hadi Inchi) kiasi ambacho hata wakitumbukia kwenye shimo la Kenge nanyi pia mtawafuata humo" tukauliza, ewe Mtume wa Allaha, una maana kuwa ni Wayahudi na Wakristo? Akajibu, kama si wao ni nani tena? (Bukhari) kutokana na hadithi hiyo tunaona kuwa kabla ya zama za mwisho kutakuwa na mielekeo mibovu ya kifikra na kimaadili na kwamba tawala zitakazokuwepo zitajitenga mbali na ukweli na haki jambo litakalosababisha mfarakano mkubwa na kuwatoa watu katika mafundisho ya Mwenyezi Mungu.

Jambo la kuzingatia hapa ni kuwa maadili ya Wayahudi na Wakristo ndio maadili ya magharibi au ya Wazungu, na mifumo ya maisha iliyojitenga na Qur'an ndio mifumo ya Magharibi inayotawala dunia hivi leo.

Muumini na Kafiri Mtume wa Mwenyezi Mungu kasema:

Kabla ya saa ya mwisho kutakuwa na vurugu vurugu tupu ambapo mtu atakuwa Muumini asubuhi na Kafiri jioni yake au atakuwa Muumini jioni na Kafiri asubuhi yake. (Abuu Daudi) Kuna vielezeo vingi vinavyoonesha hali hiyo hivi leo. Mtu anaweza kuswali swala tano lakini akawa muasherati, anaweza kushinda kutwa nzima anaswali lakini usiku anazini, anaweza kushinda na swaumu kutwa nzima lakini usiku yuko na hawara au kimada, mwingine anaweza kuwa sala tano lakini muongo, mwizi, tapeli, mla rushwa, mla riba na kadhalika. Mseto huu wa Uumini na Ukafiri unaonekana kwa watu wengi hivi leo japo kwa sura tofauti.

Kutozingatia halali na haramu Dalili nyingine ya kiama ni kuwa watu hawatazingatia yaliyoharamishwa na Mwenyezi Mungu katika Qur'an. Mtume (s.a.w.w) kasema: Utafika wakati ambapo mtu hatojali kama vitu avipatavyo ni vya halali au ni vya haramu (Bukhari).

Wanazuoni wenye nyuso mbili Mtume (s.a.w.w) kasema:

Katika zama za mwisho baadhi ya watu wanaokubalika kama wanazuoni watakuwa wanafiki kweli kweli wenye nyuso mbili; Mbwa Mwitu watasoma katika zama za mwisho. Wale watakaoziona zama hizo waombe nusra kwa Mwenyezi Mungu kutokana na uovu wa wanazuoni hao. Kutakuwa na mafisadi kweli kweli. Unafiki ndio utakaoshitadi. (Tirmidhi, Nawadil al Usul.)

Kutatokea watu katika zama za mwisho ambao watajinufaisha kwa kutumia dini (Tirmidhi) Kutumia dini kwa malengo ya kidunia Mtume wa Allah kasema;

Katika zama za mwisho watu wataitumia dini kitapeli kwa malengo yao ya kidunia na kujivika ngozi za kondoo hadharani kuonesha unyenyekevu. Ndimi zao zitakuwa tamu kama sukari lakini nyoyo zao zitakuwa nyoyo za Mbwa mwitu. (Tirmidh).

Watu hawatoheshimu mipaka ya sheria za Kiislamu. Hawatochelea kuutumia Uislamu kwa ajili ya kujipatia maslahi yao. Watu watajali zaidi kuonekana wanatenda mambo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wakiwa hawana chembe ya wema, huruma na usaidizi kwa wanaowahubiria. Watakuwa wakiwakamua wafuasi wao kutoa kwa kutumia aya na mahubiri ya kukhofisha na kutumainisha hali yakuwa wao wenyewe hawana ukweli katika nafsi zao.

Katika zama za mwisho za umma wa walioamini, watu watapamba Misikiti lakini wataziacha nafsi zao katika maangamizi, watu ambao watashindwa kuitunza dini ya Mwenyezi Mungu kama wanavyozitunza nguo zao, watatelekeza majukumu ya dini yao kwa sababu ya shughuli zao, watu hawa watakuwa wengi.

9

# DALILI ZA KIAMA

## KUTOTEKELEZA AMRI YA KUTENDA MEMA NA KUEPUKA MABAYA

Miongoni mwa dalili za kukaribia kiama ni kuwa watu wanaojua kuwa Mwenyezi Mungu amewaamrisha kutenda mema na kuepuka uovu hawatatekeleza jambo hilo: Siku ya mwisho haitasimama mpaka watakapobakia watu ambao hawatajali mema na kamwe hawatozuia maovu (Ahmad).

Karibu na kusimama kwa kiama mambo mema yatapungua (Bukhari) Katika hadithi nyingine inabainishwa dalili ya kiama kuwa Waislamu walioamini watadhoofishwa kwa msukumo wa watenda dhambi:

Saa itafika pale sauti zitakapopazwa misikitini (Tirmidh) Saa itafika pale viongozi watakapokuwa madhalimu (Al Haithami, Kitab al Fitan)

Mtume (s.a.w.w) kasema:

katika zama za mwisho, kutakuwa na watu wachache sana wanaoweza kuitwa waumini: Utafika wakati kwa watu wangu ambapo misikiti itajaa watu lakini watakuwa hawana muongozo sahihi (Ibn Babuya, Thawab ul A'mal Hadith moja inasema kuwa waislamu wa kweli watalazimika kuficha imani zao na kufanya ibada kwa siri:

Wakati utafika ambapo wanafiki wataishi kwa siri miongoni mwenu na wenye imani watajaribu kuhuisha dini yao kwa watu wengine Katika Hadith ifuatayo inabainishwa ishara ya zama za mwisho kuwa Misikiti itafanywa sehemu za mikusanyiko ya kijamii tu. Utafika wakati ambapo watu watatumia misikiti kama vijiwe tu vya kukutania. Katika zama mwisho, watatokea watu watakaosoma Qur'an kwa ajili tu ya kujinufaisha badala ya kupata radhi za Allah:

Na aombe thawabu kwa Allah yule asomaye Qur'an. Kwa sababu katika zama za mwisho kutakuwa na watu wengi watakaosoma Qur'an na kutafuta malipo kwa watu wengine. (Tirmidhi). Dalili nyingine ni kuwa Qur'an itasomwa kwa ajili ya kujifurahisha (kujiburudisha) tu kama vile wimbo:

Wakati Qur'an itakaposomwa mithili ya uimbaji wa nyimbo na wakati mtu atakapoheshimika (atakaposifika) kwa kuimba namna hiyo hata kama hana ilimu ( Al-Tabarani, Al-Kabir) Baadhi ya watu watakaotambuliwa kama Waislamu watakuwa na uelewa potofu juu ya kadari, wakati ambapo wengine wataamini nyota kuwa zinaweza kuwapatia ujuzi wa kujua maisha yao ya baadae. Hii ni dalili ya zama za mwisho:

Saa itafika wakati watu watakapoamini nyota na kukanusha Qadari (Al-Haythami, Kitab al Fitan) Licha ya ukweli kwamba Mwenyezi Mungu ameharamisha riba hivi leo riba ndio mtindo wa maisha. Katika Hadith ifuatayo hii inaelezewa kama dalili mojawapo ya ya kiama:

Bila shaka kitakuja kipindi ambacho hakuna hata mtu mmoja atakayesalimika na riba. Endapo mtu ataepuka riba kwa njia ya moja kwa moja basi hatoweza kuukwepa moshi (athari) utakaotokana nayo. Kwa kiasi fulani athari zake zitamfika tu. (Imesimuliwa na Abu Huraira)

Hapa labda tutoe ufafanuzi kidogo. Katika ulimwengu wetu wa leo riba imejikita katika mifumo ya fedha na uchumi wa kitaifa na kimataifa. Aidha

sekta za kiserikali na binafsi zinashiriki katika uchumi wa riba. Mabenki na makampuni binafsi ya kitaifa na kimataifa hasa yale yanayoendesha shughuli za ukopeshaji wa fedha au bidhaa yanatoza riba kwa viwango mbalimbali. Karibu Asasi zote za utoaji wa mikopo ya fedha zinatoza riba.

Kwa hali hiyo hakuna mtu ambaye anaweza kudai kuwa yeye amesalimika na riba. Maadam mfumo wa uchumi wa Taifa haukusalimika na riba basi sote tunahusika na jambo hili. Hivyo hadithi ya Mtume (s.a.w.w) inawafikiana kabisa na mazingira yetu.

Dalili nyingine ya zama za mwisho ni kuwa Hija itafanywa kwa ajili ya kusafiri tu, kufanya biashara, kujionesha tu na kuombaomba. Wakati huo utafika pale matajiri watakapokwenda Hija kwa malengo ya kusafiri kwa minajili ya kujifurahisha, biashara, kujifaharisha na kujionesha, na masikini kwenda kuomba. Imesimuliwa na Anas (r.a )

Tatizo kubwa ambalo Wanaadamu wanakabiliana nalo hivi leo ni kusambaratika kwa jamii. Kuporomoka huku kwaonekana katika vipengele mbali mbali vya maisha. Kuvunjika kwa familia, ongezeko la talaka na uzazi haramu ndio mambo ambayo yanapelekea kusambaratika kwa taasisi ya familia. Maisha hivi leo yamekuwa ya misukosuko, mashaka, huzuni, wasiwasi na vurugu tupu. Watu waliokosa maadili ya kiroho wanaona kuwa ili kuondokana na adha ya dunia basi bora wajitumbukize katika ulevi wa pombe na dawa za kulevya. Wengine wanaona kuwa hakuna ufumbuzi wa hali ngumu inayowakabili basi njia wanayoona itawatowa matatizoni ni kujinyonga. Moja ya Ishara kubwa za kuanguka kwa jamii ni kule kuongezeka kwa mambo ya haramu.

Kiwango cha uhalifu kimeongezeka kwa kiasi kinachowashangaza mabingwa wa maswala ya jamii. Ripoti ya uhalifu na haki ulimwenguni, "Universal Crime and Justice," Iliyotayarishwa na kituo cha udhibiti wa jinai cha umoja wa mataifa, United Nations' International Crime' imetoa tathmini ya jumla ya uhalifu ulimwenguni. Ripoti hiyo inasema:

Kimsingi, kama ilivyokuwa katika miaka ya themanini, kiwango cha uhalifu pia kiliendelea kuongezeka katika miaka ya tisini. Kila mahali ulimwenguni, katika kila kipindi cha miaka mitano, theluthi moja ya watu wanaoishi mijini wamekumbwa na mikasa ya uhalifu. Kote ulimwenguni vitendo vya wizi, ujambazi, utapeli, uasherati vimekuwa vikiongezeka siku hadi siku. Matukio haya, pamoja na sababu nyinginezo, yamekuwa yakihusishwa na athari mbaya za kiuchumi.

Kiwango cha utumiaji wa dawa mbali mbali za kulevya nacho kimeongezeka katika miaka ya karibuni. Watu hasa vijana wamekuwa wakibwia unga na kujidunga sindano zenye dawa za kulevya. Kwa kweli tatizo hili limeleta madhara ya kiafya, athari mbaya za kifamilia na kijamii.

Kwa hakika sababu za matatizo yote haya zimeelezwa katika Qur'an pale inaporejea historia ya jamii zilizopita. Kuporomoka kwa jamii na matatizo mbali mbali ni matokeo ya wanadamu kumsahau Mwenyezi Mungu na lengo halisi la maisha na hivyo kuyatupa maadili ya kiroho.

Matukio yote ya kuporomoka kwa jamii tunayoyashudia hivi leo tayari yalikwishabashiriwa na Mtume (s.a.w.w) karne 14 zilizopita. Mtume (s.a.w.w) amesema kuwa miongoni mwa dalili za zama za mwisho ni pale watu watakapokabiliana na vita na mabadiliko ya kijamii (Ahmad Diya"al

diin al Kamush Khanawi, Ramuzi al ahadith). Zifuatazo ni hadith zinazohusiana na awamu ya kwanza ya zama za mwisho:

Kutakuwa na miaka ya udanganyifu ambapo mtu mkweli hatoaminiwa na muongo ataaminiwa (Ibn Kathir). Kutakuwa na miaka ya vurugu. Watu watamuamini muongo na kutomuamini yule anayesema ukweli. Watu hawatamuamini mtu mkweli na watamuamini yule ambaye ni fisiki. (Ahmad). Siku ya kiama haitakuja mpaka watu duni kabisa wawe watu wenye furaha kabisa (Tirmidh).

Kama inavyosomeka katika hadithi hizo kutakuwa na ongezeko la watu waovu ambapo wale wanaoonekana wakweli kumbe ni waongo na wale wanaoonekana waongo kumbe ndio wakweli. Hizi ni dalili za zama za mwisho. Hadithi moja inabainisha kuwa kutakuwa na watu wachache sana wakweli na kiasi kidogo sana cha pesa kitakachopatikana kwa kuzingatia kanuni na sheria za dini yetu:

Katika zama za mwisho watu watakuwa wakifanya biashara lakini hakutakuwa na mtu yeyote mkweli (Bukhari na Muslim). Ushahidi wa kweli utatupiliwa mbali na ushahidi wa uongo na kusingiziana ndivyo vitakavyoshamiri. Hii ni dalili nyingine ya zama za mwisho. Kwa hakika katika saa ya mwisho kutakuwa na ushahidi wa uongo na ufichaji wa ushahidi (Ahmed na Hakim). Kutakuwa na shutuma za uongo za mambo machafu na masingiziano. (Tirmidh)

Kigezo pekee ambacho kwacho watu watapimwa ubora wao ni mali, hashima itategemea mtu ni tajiri kiasi gani:

Kabla ya saa ya mwisho kufika, kutakuwa na salamu maalumu kwa watu wa tabaka fulani. (Ahamad) Hakutakuwa na hukumu mpaka pale salamu zitakapotolewa sio kwa watu bali kwa watu mahususi. (Mukhtasari Tazkira Khutub). Inasemwa katika hadithi kuwa dalili nyingine ni kuvurugika kwa uhusiano wa kijamii baina ya watu:

Ni wale watu ambao mtu anawajuwa tu ndio watakaopewa salamu (Ahmad Diyal al diya'al Din al Kamushi Khanawi, Ramuzi al ahadithi) Katika hadithi ifuatayo inaelezwa kuwa nafasi za kazi zitatolewa kwa watu wasio na sifa: Pale madaraka na mamlaka yatakapokwenda mikononi mwa watu wasio na sifa, basi hapo muisubiri ile saa (kiama). (Bukhari). Dalili nyingine ya zama hizo itakuwa ni kuvunjika kwa uhusiano wa wanafamilia, marafiki, majirani na kuvurugika kwa jamii na maadili:

Mtu kutokuwa na mapenzi na Mama yake na kumfurusha Baba yake (Tirmidh). Kwanza kutakuwa na sokomoko kwa mtu kuhusiana na familia yake, mali yake, nafsi yake, watoto wake, jirani zake (Bukhari na Muslimu).

Dalili nyingine ya zama za mwisho ni kuwa vijana watakuwa waasi na mapenzi na heshima kati ya vijana na wazee vitapungua: Wakati wazee watakapokosa huruma kwa vijana, na wakati vijana watakapokosa heshima kwa wazee Watoto watakapokuwa na jazba Basi hapo hukumu ipo jirani.

(Imeripotiwa na Umar (r.a)). Hadithi nyingine zinaonyesha dalili nyingine ya zama za mwisho kuwa talaka na idadi ya watoto wa nje ya ndoa vitaongezeka: Talaka itakuwa ni jambo la kila siku (Allamah Safarini, Ahwal Yaum al Kiyama). Kutakuwa na wingi wa watoto wa haramu (Al Muttaqi Al Hindi, Muntakhab Kanzul Ummaal).

Kwa kutenzwa na itikadi ya Ulahidi na mtazamo wa kidunia, watu wataikumbatia dunia kupindukia na wataghafilika na maisha ya akhera. Hii ni dalili nyingine ya zama za mwisho: Uchoyo na Uroho utaongezeka. (Muslim, ibn Majah). Wakati huo, watu wataiuza dini yao kwa kiasi kidogo cha maslahi ya dunia (Ahmad). Hadithi nyingine inasema kuwa watu watalaaniana na kuapizana: Katika siku za mwisho kutakuwa na watu ambao pale wakutanapo hulaaniana na kutukanana badala ya kusabahiana (kwa salamu) (Allama) (Jalaludiin) Suyuti, Durre Mansouri). Dalili nyingine ya zama hizo ni utesi na dharau kwa watu wengine:

Kutakuwa na wingi wa wasutaji, vizabizabina, Wambea, wagombanishaji, waamsha fitina na watu wenye dharau katika jamii. (Al Mutaqi Al Hindi, Muntakhab Kanzul Ummaal) Dalili nyingine ya Kiama ni rushwa:

Udanganyifu na ulaghai yatakuwa mambo ya kawaida (Allama Safarini Ahwal Yaum al Qiyama) Rushwa itaitwa zawadi na itaonekana kama halali tu: (Ammal Al diin al Qazwini, Mufid al ulumi wa Mubid al Humum). Mtume (s.a.w.w) kasema, mauaji yataongezeka sana katika zama za mwisho: Kiama hakitasimama hadi pale mauaji yatakapozidi. (Bukhari).

10

# DALILI ZA KIAMA

## KUKUA KWA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Mtume Muhammad(saw), kama sote tujuavyo aliishi karne kumi na nane zilizopita. Kumbukumbu za Historia zinaonesha kuwa wakati Qur'an ilipofunuliwa jamii ya Waarabu haikuwa na teknolojia ya kuwawezesha kufanya tafiti za dunia au ulimwengu.

Kwa sababu hiyo kuna tofauti kubwa kati ya kiwango cha sayansi na Teknolojia cha wakati wa alioishi Mtume (s.a.w.w) na wakati huu wetu. Tofauti hii ilianza kuwa kubwa hasa zaidi mwanzoni mwa karne ya ishirini. Kielezeo cha wazi cha hilo ni mageuzi makubwa ya kiteknolojia yanayoonekana katika wakati wetu huu ambayo, hayakupata kuonekana sio tu wakati wa Mtume bali hata katika miongo michache iliyopita. Licha ya tofauti hiyo, bado katika karne ya saba Mtume(s.a.w) alizungumzia mambo mengi ya hakika juu ya maisha. Hapa tutaziangalia Hadithi zinazoelezea kiwango cha maarifa ya sayansi na Teknolojia katika zama za mwisho. Tutaona kuwa yale aliyoyabainisha Mtume (s.a.w.w) karne kumi na nne zilizopita yanadhihirika leo.

Elimu Tofauti kubwa inayobainika kati ya krne za 20 na 21 na zama zilizopita ni kuongezeka kwa mwamko wa elimu. Huko nyuma uwezo wa kusoma na kuandika ulihodhiwa na watu wachache. Lakini kuanzia mwishoni mwa karne ya ishirini UNESCO na taasisi za serikali pamoja na mashirika binafsi yamefanya kazi kubwa ya kusambaza elimu.

Kwa mujibu wa ripoti ya UNESCO, kiwango cha elimu ya kujua kusoma na kuandika kilifikia asilimia 77.4 mwaka 1997. Kiwango hiki ni kikubwa mno. Mtume (s.a.w.w) aliielezea hali hii kama ni dalili mojawapo ya zama za mwisho; "Mwamko wa elimu(literacy) utaongezeka pale hukumu inapokaribia"(Ahmad Diyaal-Din-Alkhamush Khanawi, Ramuz-al-Ahadith). i

Teknolojia ya ujenzi Dalili nyingine ambayo Mtume (s.a.w.w) ameitaja kuhusiana na zama za mwisho ni ujenzi wa maghorofa marefu:

"Hakutakuwa na hukumu hadi pale maghorofa marefu sana yatakayojengwa"(imesimuliwa na Abu Huraira) "Kiama hakitasimama mpaka watu washindane kujenga maghorofa marefu.(Bukhari)

Tukiingalia historia ya usanifu majengo na uhandisi, tunaona kuwa maghorofa mengi marefu yalianza kujengwa na mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Maendeleo ya Teknolojia kuongezeka kwa matumizi ya chuma cha pua na matumizi ya Kambarau(lifti za kupandia maghorofani) kumeongezeka kasi ya ujenzi wa maghorofa. Maghorofa marefu yameshamiri kweli kweli hivi leo. Alichokisema Mtume (s.a.w.w) katika Hadithi kinadhihirika wazi wazi. Watu na mataifa yanashindana kuongeza maroshani ya ghorofa.

Teknolojia ya usafiri Katika historia yote, kumekuwa na uhusiano kati ya maendeleo na mawasiliano. Jamii ambazo zimeweza kujiwekea miundo mbinu bora ikiwa ni pamoja na mifumo bora ya usafiri zimejipatia maendeleo. Akizungumzia dalili za zama za mwisho, Mtume (s.a.w.w) kayataja maendeleo ya usafiri. "Kiama hakitasimama hadi muda utakapopita

upesi upesi (Bukhari) Masafa ya mbali mno yatafikiwa kwa muda mfupi.(Ahmad Musnad)

Ujumbe unaobebwa na Hadithi hiyo unadhihirika wazi wazi hivi leo. Katika zama hizi masafa ya mbali yanafikiwa kwa muda mfupi tu. Madege, magari na Treni ni vyombo vinavyoweza kusafiri masafa ya mbali kwa muda mfupi. Huko nyuma safari za masafa marefu zilichukua miezi. Qur'an pia inavielezea vyombo hivi:

"Na amewaumbia Farasi na nyumbu na punda ili muwapande na (wawe) mapambo. Na ataumba vipano) msivyovijua (6:8).

Hebu tuutafakari huu usemi wa muda utapita upesi upesi katika ile hadithi ya kwanza. Kwa kuzingatia yale tuliyoyaeleza, ni wazi kama Mtume (s.a.w.w) alivyonena kuwa katika zama za mwisho, kazi zitafanywa kwa muda mfupi kuliko zilivyokuwa zikifanywa huko nyuma.

Kwa kweli maendeleo ya sayansi yamewezesha mambo mengi kutimizwa kwa muda mfupi zaidi. Hadithi hiyo hiyo inathibitisha jambo hili: Kiama hakitakuja kabla muda kupungua. Mwaka uwe kama mwezi, mwezi uwe kama wiki na wiki iwe kama siku (Tirmidh).

Mathalani zama zilizopita, mawasiliano ya kimataifa yalichukua majuma mengi lakini sasa yanafanyika kwa sekunde tu kwa tovuti na teknolojia nyinginezo za mawasiliano. Kurahisishwa kwa mawasiliano kumewezesha chombo cha anga cha Marekani kutumwa katika sayari Mars zaidi ya maili milioni 106 ambacho hivi kinaendelea kuleta taarifa mbali mbali za kiuchunguzi duniani pamoja na picha kwa muda mfupi sana.

Katika zama za nyuma bidhaa zilifika kule zilikopelekwa baada ya safari ndefu za miezi, hivi leo zinafika mapema kabisa. Hivi sasa mamilioni ya vitabu yanaweza kuchapwa kwa muda uliotumika kuchapwa kitabu kimoja karne chache zilizopita. Katika masuala ya afya na njia za utayarishaji wa vyakula hapahitajiki tena muda mrefu wa kushughulikia kutokana na Teknolojia ya sasa.

Unaweza kutoa mifano mingi mno. Hata hivyo tumalizie hapa kwa kusema kuwa dalili zote alizozieleza Mtume (s.a.w.w) katika karne ya saba zinaonekana wazi wazi hivi sasa. Dalili nyingine aliyoitaja Mtume (s.a.w.w) ni kuongezeka kwa biashara, kama iliyoripotiwa na Ibn Mas'uud(r.a). Biashara inakwenda pamoja na maendeleo ya Teknolojia na usafirishaji wa kisasa umeiwezesha kila nchi duniani kujenga uhusiano na ushirikiano wa karibu wa kibishara na nchi nyingine.

11

# DALILI ZA KIAMA

## TEKNOLOJIA YA MAWASILIANO

Baadhi ya Hadithi za Mtume (s.a.w.w) zimeelezea Teknolojia ya leo ya mawasiliano;

"Saa ya mwisho haitafika kabla jumbe hajasemeshwa na fimbo yake.(Tirmidh)

Tukiiangalia hadithi kwa makini, twaweza kuona ukweli uliomo ndani yake. Katika zama zilizopita fimbo ilitumika kuendeshea wanyama wa kupanda hasa hasa ngamia na farasi. Hapa tunaona Mtume (s.a.w.w). Hapa tunaona Mtume (s.a.w.w) ametumia tamathali.

Hebu tujiulize ni kitu gani kinachosema ambacho twaweza kukilinganisha na fimbo kwa sifa za maumbile? Jibu la kwamza laweza kuwa simu. Au vyombo vingine vya mawasiliano. Vyombo vya mawasiliano visivyotumia waya kama vile simu za mkononi na simu za upepo kama sattilaiti ni vyombo vya hivi karibuni kabisa. Kwa kuvitazama vyombo tutaona wazi wazi kule kutimia kwa bishara ya Mtume (s.a.w.w) iliyotolewa miaka 1400 iliyopita. Kwa hivyo huu ni ushahidi kuwa zama zetu ziko jirani na siku ya hukumu. Katika Hadithi nyingine Mtume (s.a.w.w) anaelezea maendeleo ya Teknolojia ya mawasiliano:

"Hakutakuwa na hukumu mpaka sauti ya mtu imsemeshe yeye mwenyewe(Hadi mtu asemeshwe na sauti yake.(Mukhtasar Tazkira; Allama Qurtubi). Ujumbe wa Hadithi hii unathibitika hivi leo.Ili mtu aisikiye sauti yake kwanza hurekodiwa na kisha kusikilizishwa. Teknolojia ya kunasa na kutoa sauti ni ya karne ya ishirini. Huu ndio ulikuwa mwanzo wa maendeleo ya sayansi ambayo ndio imezaa vyombo vya mawasiliano na habari. Unasaji wa sauti sasa umefikia kiwango cha juu kutokana na matumizi ya kompyuta.

Kwa kifupi vyombo vya elektroniki vya hivi leo kuna vipaza sauti ambavyo vimewezesha mtu kujinasa na kujisikia sauti yake mbali ya kanda za rekodi na vionesho vya picha(video). Hii inadhihirisha kuwa Hadithi ya Mtume iliyonukuliwa hapo imetimia. Kwa hiyo hii ni dalili nyingine ya kiama. Si hadithi hizo tu bali kuna ishara nyingine zilizotajwa na Hadithi zifuatazo:

Mkono utanyooshwa kutoka angani na watu watautazama na kuuona.(Ibn Hajar Haythami, AlQawl al Mukhtasar fil alamat al Mahdi al Muntanzir. Dalili ya siku hiyo mkono kunyooshwa angani na watu kuacha kuangalia.(Al-Muttaqil al Hindi, AlBurhan fi Ahmad al-Mahdi Akhir al-Zaman)

Ni dhahiri kuwa neno "mkono" katika hadithi hiyo limetumika kwa tamathali. Katika zama zilizopita neno hili huenda halikueleweka zaidi. Lakini ikitazamwa teknolojia ya leo, kauli yaweza kutafsiriwa kwa namna nyingi. Kwa mfano Televisheni ambayo imekuwa sehemu muhimu ya maisha ya leo pamoja na kamera na Kompyuta zaweza kubeba tafsiri ya kauli hiyo.

Neno "mkono" yawezekana limetumika likiwa na maana ya uwezo. Yaweza kuwa na maana pia taswira zinazotoka angani kwa sura ya mawimbi ambayo ni televisheni:

"Sauti itamwita mtu kwa jina lake na hata watu wa magharibi na mashariki watasikia.(Ibn Hajar Haythami, Al Qawl al Mukhtasar fi alamat ala Mahdi al Muntazar). Sauti hii itavuma itaenea duniani kote na kila kabila litaisikia kwa lugha yao wenyewe(Al-Muttaq al Hindi, al Burhani fi alamat al Mahd Akhir al Zaman).

Sauti kutoka mbinguni ambayo kila mtu ataisikia kwa lugha yake. (Al-Muttaq al Hindi, al Burhani fi alamat al Mahd Akhir al Zaman). Hadithi hapa zinataja sauti ambayo itasikika dunia nzima na kwa lugha ya kila mtu. Ni dhahiri hii ina maana ya Radio, Televisheni, simu za mikononi na nyenzo nyingine za mawasiliano. Huu ni muujiza kwamba Mtume(s.a.w) alitaja maendeleo ambayo hayakufikirika katika kipindi cha miaka mia moja tu iliyopita. Mfasiri maarufu Badiuzzaman wakati akifasiri hadithi hizi alieleza kuwa, zimebashiri kimiujiza kuja kwa radio, televisheni na vyombo vingine vya aina hiyo.

Kuzuka kwa manabii wa uongo Inafahamika kuwa katika kipindi chote cha historia, kumekuwa na manabii wengi wa uongo. Katika hadithi inabainishwa kuwa Manabii wa uongo watazuka kabla ya siku ya hukumu. Saa ya mwisho haitafika kabla ya kuja kwa Madajali(Wadanganyifu) thelathini kila mmoja akijitambulisha kama nabii wa Allah.(Abu Dawood) Kwa kutumia fursa ya matazamio ya Waislamu na itikadi ya dini ya kikristo kuwa Nabii Isa au Yesu atarejea, idadi kubwa ya watu wadanganyifu wamejitokeza kudai unabii.

Kumbukumbu zinaonesha kuwa , Manabii wa uongo walianza kujitokeza katika miaka ya 70. Ifuatayo ni baadhi ya mikasa iliyotokana na madai ya unabii yaliyojitolewa na watu mbali mblia katika nchi mbali mbali. Maafa ya moto; David Koresh na wafuasi wake wapatao 74 katika eneo la Waco, Texas walikufa kwa kujiwasha moto.

Wiki moja kabla ya hapo maeneo mawili ya Uswisi na moja nchni Canada, walikufa jumla ya Wafuasi 53 wa Jouret, wakiwemo na watoto wao. Polisi katika nchi hizo mbili wanafanya uchunguzi kujua kama vifo hivyo ni vya kujiua, kuuawa au yote mawili kutokana na imani za ajabu.

Sun Myung Moon, mwasisi wa Kanisa la Unification anadai yeye ni Masihi aliyekuja kwa mara ya pili. Kanisa la Unification lilianzishwa rasmi na Moon mnamo mwaka 1954. Moon anadai kuwa mwaka 1936 yeye alipokuwa na umri wa miaka 16, Yesu alimtokea upande wa mlimani kaskazini magharibi mwa Korea na kumwambia kuwa Mungu amemchagua kwa kazi ya utume wa kusimamisha Ufalme wa mbinguni na ardhini.

Zaidi ya watu 1000 wahofiwa kufa baada ya kugundulika kwa makaburi mengi zaidi nchini Uganda. Hao walikuwa wafuasi wa mtu aliyedai kuwa nabii Kibwetere. Zaidi ya watu 900, wafuasi wa dhehebu moja, walikutwa wamekufa pamoja katika msitu wa Amerika kusini. Watu wote waliokufa walikuwa wafuasi wa Mchungaji Jim Jones, kiongozi wa hekalu mjini San Francisco.

Qur'an pia inaeleza kuja kwa mnabii wa uongo; Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule amtungiyae uongo Mwenyezi Mungu au mwenye kusema: Nimeletewa Wahyi", na hali hakufunuliwa chochote; na yule asemaye: Nimeteremsha(ufunuo) kama ule aliouteremsha Mwenyezi Mungu. Na kama ungewaona madhalimu watakapokuwa katika mahangaiko ya mauti na malaika wamewanyooshea mikono(kuwaambia) zitoeni roho zenu! Leo mtalipwa adhabu ifedheheshayo kwa sababu ya yale mliyokuwa mkizifanyia kiburi Aya zake(ungeona namna gain wanavyopapatika) (6:93).

Kama inavyoelezwa katika aya hiyo watu hawa wazushi kwa hakika watapata malipo yao kwa uongo waliozusha. Hapana shaka kuwa utafika wakati ambapo uongo wote wa manabii wa uongo utafutiliwa mbali. Mtume(s.a.w) akasema kuwa baada ya warongo hawa kuondoka ndipo Isa (s.a) atakapokuja tena.

Kama tulivyoeleza kurasa za nyuma kuwa Qur'an inatufahamisha kurejea kwake duniani, na kwamba Waislamu na Wakristo, kwa hamu, wanasubiri ujio wake, kuna Hadithi chache za Mtume (s.a.w.w). Mwanazuoni wa kiislamu Shawkani kasema kuwa kuna Hadithi 29 zinazoelezea kurejea kwa Issa na kwamba maelezo yaliyomo katika hadithi hizi hayawezi kupotoshwa.(Ibn Majah)

Kuna jambo moja muhimu linalotujia kutokana na Haithi hizi. Kurejea kwa Isa kutatokea awamu ya pili ya zama za mwisho na ndio itakuwa ishara muhimu(dalili kuu) ya siku ya hukumu. Hadithi zinazohusiana na jambo hili ni hizi;

Saa ya mwisho haitafika mpaka muone mshuko wa Issa (a.s) mwana wa Mariamu (Muslim). Naapa kwa yule ambaye roho yangu iko mikononi mwake. Mwana wa Maryamu, muda si mrefu atashuka miongoni mwenu (Waislamu) kama mtawala mwadilifu wa haki(Bukheri).

Saa haitasimama hadi pale atakaposhuka mwana wa Maryamu miongoni mwenu kama mtawala mwadilifu(Bukhari) Mtume (s.a.w.w) anatueleza kile atakachofanya Isa pale atakaporejea; unapowadia wakati wa kifo chake Isa atakuwa ameonekana tena duniani kwa kipindi cha miaka 40.(Abu Dawuud).

Isa (a.s) mwana wa Maryamu atashuka kutawala kwa miaka arobaini kwa kitabu cha Allah na kwa Sunna yangu hadi anapokufa. (Al-Muttaqi al Hindi, Al Burhani fi Alamat al Mahdi Akhir al zaman)

12

# DALILI ZA KIAMA

## ZAMA BORA

Sifa za zama bora zilizoelezewa kwa kina na Mtume (s.a.w.w) ni dalili muhimu ya siku ya hukumu. Kipindi hicho kinachoitwa "Golden age" kitakuwa bora kwa sababu ya kule kulinganishwa kwake na pepo kwa maelezo ya Mwanachuoni wa kiislamu.

Imeelezwa katika Hadithi kuwa zama hizo bora zitakuwa katika awamu ya pili ya zama za mwisho. Sifa moja kuu ya kipindi hiki cha furaha itakuwa ni ule utajiri wake mkubwa wa mali. Hadithi zinasema kuwa utajiri huo hautakuwa na mfanowe katika historia:

Umma wangu utapata hali bora katika zama hiyo ambayo mfano wake haujapata kuonekana hapo kabla (ibn Majah). Umma wangu wa wema na wabaya utaneemeshwa neema ambazo haukupata kuziona kabla (Al-Muttaq al Hind Al Burhan fi Alamat al Mahd Akhira Zaman).

Hadithi nyingine inaelezea utajiri wa zama hizo: Katika kipindi hicho, ardhi itatupa nje hazina yake.(Ibn Hajar Haythami, AlQawli al Mukhtasar fii alamat al Mahdi al Muntazar) Hadithi nyingine zinaelezea kuwa miaka ya mashaka na huzuni itakwisha. Hakuna mtu atakayekuwa katika shida. Hakuna mtu atakayetakiwa kutoa zaka.

"Toeni zaka kwani utakuja wakati ambapo mtu atakwenda na zaka yake huku na kule asipate mtu wa kuipokea (Bukhari). Kwa hakika bidhaa zitakuwa nyingi na zitamwagika kama maji lakini hakuna atakayeziokota(Al Halimi). Sifa nyingine ya zama bora itakuwa ni kushitadi kwa haki na ukweli. Utakuwa wakati ambapo sheria na haki zitachukua nafasi ya hofu, mfarakano na dhuluma.

Kama tunavyosema katika Hadithi, dunia itajaa haki badala ya ukandamizaji na mateso (Ahmad Diya'al Din al Kamushkanawi, Ramuz al Ahadithi) Miongoni mwa sifa bora za kipindi hicho ni kunyamaa kwa silaha(kutulia kwa milio ya silaha), kutoweka kwa uadui, migogoro na kukoma kwa misambaratiko ya kijamii. Badala yake kutashamiri urafiki na mapenzi miongoni mwa watu. Kiasi kikubwa cha pesa kilichotumika kugharimia vita na viwanda vya silaha sasa kitawekezwa kwenye chakula, afya, maendeleo, utamaduni na mambo yatakayoleta furaha kwa watu wote.

Sifa nyingine ya kipindi hiki cha neema itakuwa ni kurejea katika misingi ya dini ya Mwenyezi Mungu kama ilivyofundishwa na Mtume (s.a.w.w). Zile sheria na mila zilizobuniwa baada ya Uislamu zitaondoshwa. Tafauti za Waislamu katika kuitekeleza dini yao zitakoma.

Kwa kifupi, zama bora ni kipindi cha neema nyingi, maisha bora, amani furaha, utajiri na faraja. Utakuwa ni wakati ambao maendeleo katika sanaa, tiba, mawasiliano, uzalishaji, usafirishaji na katika maeneo mengine ya maisha yatakuwa katika sura ambayo haikuwahi kuonekana katika historia ya dunia. Na watu wataishi kwa kuzingatia mafundisho ya Qur'an.

Baada ya zama bora Tunaposoma habari za Mitume katika Qur'an tunaona kuwa kanuni ya Mwenyezi Mungu imefanyakazi katika zama zote. Jamii zinazomkadhibisha Mtume wa Mwenyezi Mungu na kumpiga vita basi huishia kuangamizwa. Lakini wale wanaomtii Mtume hupata neema

nyingi za kidunia na Ustawi wa Kiroho ambao dini sahihi huwaletea. Lakini baada ya kupita mitume hawa, baadhi ya Watu huanza kukengeuka na kuikanusha dini sahihi kuanza kuishirikisha na Mwenyezi Mungu.

Mifarakano na migongano hutokea. Kwa kweli watu wa jamii hizi wamejikuta wakiangamia kwa mikono yao wenyewe. Kanuni, hapana shaka, itafanya kazi katika zama za mwisho. Mtume (s.a.w.w) amebainisha kuwa kiama kitakuja baada ya kifo cha Isa(a.s) na mwishoni mwa zama bora kama tulivyosoma.

"Baada ya yake (Nabii Isa) siku ya hukumu itakuwa jambo la muda mfupi mbele  (Ahmad Diy'aal Din al Kamushkanawi, Ramuz Al Ahadith). Siku ya hukumu itakuja baada yake (Nabii Isa) ( Ahmad Diy'aal Din al Kamushkanawi, Ramuz Al Ahadith.

Hapana shaka zama mwisho na zama bora vitakuwa vipindi ambapo onyo la mwisho litatolewa kwa Wanaadamu. Hadithi nyingi zinaelezea kuwa hapatakuwa na mema baada ya kipindi hiki.

Hivyo tunaona kuwa muda mfupi baada ya kifo cha Isa (a.s) watu duniani watakuwa waovu na wataitupa dini sahihi. Ule wingi wa mali katika zama bora utawazuzua na hivyo kuharibikiwa. Hapa twaweza kusema kuwa katika mazingira haya ndipo kiama kitakapotokea lakini Allah ndiye ajuaye.

Kwa jinsi tulivyoziona dalili za kiama, yaweza kusemwa kuwa Karne hii ya ishirini na moja inaashiria mwanzo wa enzi mpya kabisa za historia ya dunia. Tunamuomba Allah atufishe na kutufufua hali ya kuwa ni Waislamu.

## MWISHO

13

## FAHARASA


1 ....................................................DALILI ZA KIAMA
1 ................................ KIMEANDIKWA NA: HARUN YAHYA
1 .................. KIMEFASIRIWA NA: SHUAYBU HUSEIN KIFEA
3 ....................................................DALILI ZA KIAMA
3 .................................................... SAA INAKARIBIA
6 ....................................................DALILI ZA KIAMA
6 ............................................................. MITUME
9 ....................................................DALILI ZA KIAMA
9 ..................................KURUDI KWA NABII ISA DUNIANI.
14 ..................................................DALILI ZA KIAMA
14 ..............................UTAFITI WA ANAGA NA UVUMBUZI
17 ..................................................DALILI ZA KIAMA
17 ...........................................VITA NA MACHAFUKO
19 ..................................................DALILI ZA KIAMA
19 ................................ KUANGAMIA KWA MIJI MIKUU:
21 ..................................................DALILI ZA KIAMA
21 ............................................................UMASIKINI
24 ..................................................DALILI ZA KIAMA
24 .......... KUKANUSHA DINI SAHIHI NA MAADILI YA QUR'AN
27 ..................................................DALILI ZA KIAMA
KUTOTEKELEZA AMRI YA KUTENDA MEMA NA KUEPUKA
27 .............................................................MABAYA
31 ..................................................DALILI ZA KIAMA
31 ........................KUKUA KWA SAYANSI NA TEKNOLOJIA
33 ..................................................DALILI ZA KIAMA
33 ................................ TEKNOLOJIA YA MAWASILIANO
36 ..................................................DALILI ZA KIAMA
36 ....................................................... ZAMA BORA
37 ............................................................MWISHO